Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Wote Yupo Hapa


Asante, Ndugu Borders.

2 Hebu tuendelee tu kusimama, kwa muda mfupi, kwa maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Sababu ya mimi kufanya hivi, nafikiri ni vyema kila mara kumkaribia Yeye kwanza kwa maombi. Sasa, kuna mambo mengi tunayohitaji, nina hakika, lakini hebu tuyakumbuke tu mbele za Mungu, tunapoinua mikono yetu na, moyoni mwetu, tuseme, "Mungu, nikumbuke, nina haja sasa, mimi ni . . . matarajio makuu alasiri ya leo, na kwa hiyo, tunataka Wewe utujalie hilo, Baba." Inua mkono wako sasa, kwako wewe uliye na . . . unayetarajia Mungu afanye jambo fulani.

3 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukaribia tena kwa unyenyekevu. Tunaweza tu kuona nafsi zetu zikipaa juu sasa, mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu huko, zikileta mbele yetu, Bwana, Dhabihu ye—yetu, Jina la Bwana Yesu, kuliwasilisha madhabahuni, na kukiri ya kwamba asili yetu ni wenye dhambi, Bwana. Nasi ha—hatustahili kukaribia, lakini ulitwambia tuje, nasi tungepata rehema kwa—kwa amri Yako, na kwamba maombi yetu yangejibiwa ikiwa tutaomba kwa Jina Lake. Nasi tuna mahitaji mioyoni mwetu, Bwana, kila mmoja wetu. Ee Mungu, tujalie. Na Bwana, kila mmoja wetu anaweza kukujulisha tunachohitaji. Nasi tunaweka maombi ye—yetu pamoja juu ya madhabahu Yako pamoja na Dhabihu ile ile, Bwana Yesu, na kukuomba kwamba ujibu.

4 Bwana, langu ni kwa ajili ya hawa watu alasiri ya leo, jalia jambo fulani litendeke, Bwana. Kufungwa kwa mkutano huu mkuu, Mungu, jalia usifungwe, jalia uendelee tu, Bwana, uendelee tu na kuendelea, katika kila kanisa, katika kila moyo, na usikome mpaka, Bwana, utakapomaliza nasi duniani.

Na, Baba, tunaomba ya kwamba utawajalia haja zao, kila mmoja wao, utupe shauku za moyo wetu, kwa maana ni kwa ajili ya utukufu Wako.

5 Na pia, Baba, kumbuka leo, tunapolileta Neno, jalia likolee kwa Roho, Bwana, Roho na alidhihirishe, mioyo yetu na iwe tayari kulipokea, na lianguke ndani kabisa chini ya moyo liingie nafsini, na hapo na litoe matokeo liliyokusudiwa, Bwana. Tujalie.

6 Wabariki ndugu zetu kila mahali katika siku hii ya Sabato. Kote ulimwenguni wahudumu wanahubiri Injili, Injili ii hii, tunaomba, Baba, ya kwamba utawabariki kila mahali.

7 Tunakushukuru kwa ajili ya asubuhi njema, Bwana, ibada kuu kila mahali, tunaomba ya kwamba utabariki kila mmoja, Bwana, kila kitu kilichosemwa. Sasa pata utukufu kutokana na kukusanyika kwetu alasiri ya leo, kwa kuwa tunajikabidhi Kwako pamoja na haja ze—zetu, na Neno Lako, katika Jina la Yesu. Amina.

8 Nimekuwa hudumani kwa baadhi, takriban miaka kumi na mitano katika uinjilisti. Haidhuru ni muda gani ni—niko hudumani, daima inaonekana kuwa kuna mguso wa hisia za moyoni unapofika mwisho wa mkutano. Sijawahi kuwa na mmoja bado ambapo hapakutokea hisia ndogo.

9 Muda mfupi uliopita, nilipokuwa nikienda msituni, nyuma tu ya mahali ninapokaa, basi niliwaza, "Vema, unajua kutakuwa na wengi wa watu hao ambao sitawaona tena, si—sitawaona tena duniani." Nami nafikiri, "Wakati mwingine nitakapowaona itakuwa huko Utukufuni, au ama: Vipi kama baadhi yao hawataokoka, Bwana, naye Bibi-arusi, Kanisa itabidi lisimame pale kama Hakimu?" Mnaona? "Nao watakatifu wataihukumu dunia."

10 Na pale, nikisimama pale, na kuwaangalia watu na, katika mkutano huu, nami nikawazia, "Bwana, vipi kama kitu fulani . . . ambacho ningeweza kufanya cha zaidi, kwamba kama ningalikifanya hivyo, wao—wao wange—wangekuwa sawa? Mnaona? Vipi kama ningeninii tu . . . ? Kuna kitu nimeacha?" Sikuzote linakupa hisia ya ajabu.

11 Ninatambua kwamba siku moja sina budi kusimama. Na sasa, huo hapo wakati mmoja ambapo utakutana na Hukumu, unaweza kukutana nayo sasa, ukitaka, lakini kama hutaki, itakubidi kukutana nayo kwa vyovyote vile; utakutana nayo Kule bila rehema, ama unaweza kukutana nayo sasa kwa rehema. Kwa hivyo ikiwa baadhi hapa ambao bado hawajalitatua bado, na tulitatue sasa. Mnaona? Na ikiwa mimi . . .

12 Najua katika kila mkutano mna watu wanaoingia kutoka kila mahali, kwenye mkutano huru namna hii. Kumekuwa na wale ambao wamehudhuria ambao wamekuwa wakosoaji, naweza kulihisi; ninii tu, loo, jamani, linakukera vibaya sana! Na halafu, kumekuwa na baadhi ya imani tamu sana, nyenyekevu sana ambayo nimewahi kukutana nayo maishani mwangu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Kwa hivyo unakutana na hayo kila mahali.

13 Sina hakika, ninaamini mwanamke mmoja, jana usiku, alivuka mpaka kati ya neema na rehema. Nilimwona akisimama mbele yangu, nilikuwa nikimwombea kila usiku, naye huyo hapo alikuwa amesimama pale, na weusi ukimzunguka-zunguka, haidhuru anajaribu kufanya nini, imekwisha. Na kwa hiyo mimi . . . Asubuhi ya leo, kidogo baada ya mapambazuko,

nilimwona, na mimi—mimi nilikuwa nikiomba, nikawaza, "Huyo mwanamke angewezaje kuwaza mawazo kama hayo?" Lakini nisingeweza kusaidia. Kwa hivyo nawe unawazia hayo. Nawazia, "Sijui kama kuna kitu nilichofanya, njia, au labda kama mimi . . . "

14 Nami siwezi kubembeleza chochote, hu—hupaswi kufanya hivyo, hilo ni kosa, unaona, huna budi kusema ukweli. Ukweli ni sahihi kila wakati. Na hivyo, i—inakufanya uwazie, nawe unaliwazia na kulifadhaikia.

15 Lakini na—nataka kuwashukuru, sasa, hawa ndugu wahudumu wazuri, kila mmoja wao, nanyi mnawakilisha madhehebu mbalimbali, madhehebu tofauti, na kadhalika, bali mmekuwa ndugu halisi. Nataka kila mmoja wenu ambao ni washiriki wa makanisa yao, kuwaunga mkono. Inahitaji mtu kuwakilisha *kitu fulani*, labda, wakati dhehebu lake mwenyewe . . . mashirika mengi yanazungumza . . . yanadhani ninawapinga, na mengi yao yananikataa kabisa. Na hawa hapa baadhi ya watu wao wenyewe katika mashirika hayo, hata hivyo, haidhuru mashirika yao yanafanya nini, wanaliamini, nao wanasimama kwa vyovyote vile. Hao ni—hao ni watu halisi, hao ni watu nilio na matumaini nao, mnaona, watu ambao ninaamini nitaishi pamoja nao katika Umilele. Mnaona?

16 Ningependa kujiweka wazi: kamwe siyapingi madhehebu, si madhehebu, ni mfumo wa madhehebu, mnaona, huo ndio.

17 Vipi kama ningekuona ukishuka kwenye mto huu *hapa* nje, popote pale, nafikiri kuna mto unaopitia humu mjini, na labda kuna maporomoko makubwa hapa chini, nawe uko kwenye maskini mashua ndogo inayovuja, nami najua mashua hiyo itavunjikia kwenye maporomoko hayo? Najua itavunjika, huku nami nikikupigia kelele, kukupigia makelele, si—sina neno nawe, na—na—nakupenda. Hiyo ndiyo sababu ninapiga mayowe jinsi ninavyoyapiga. Unaona? Hiyo ni . . . sio kwa sababu nina chochote dhidi ya mtu aliye kwenye hiyo mashua, mashua ndiyo ninayonena juu yake, hiyo mashua haitavuka. Wala hakuna shirika, ama dhehebu, au shirikisho, ama chochote kile, kitakachotuvusha, ni Kristo na Yeye pekee, hiyo ni kweli; na sivyo, ndugu zangu.

18 Sasa, sisi tunachukua Assemblies of God, hii ni Open Bible, Assemblies of God, Open Bible, Foursquare, mbona, jamani, Umoja wa Kipentekoate, ndugu wa Umoja, na ndugu wa Church of God, Utakatifu wa Kipentekoste, mbona wao, hao hapo baadhi ya watu wazuri sana niliowahi kukutana nao maishani mwangu mle ndani. Wao ni ndugu, Wakristo halisi waliozaliwa mara ya pili. Na kama ukiniona kuwa nina upambanuzi kidogo kutoka kwa Mungu, ninawaambia ukweli. Katika sehemu hizo zote, mimi hukutana na watu halisi wa Mungu.

19 Nami hukutana nao katika Methodisti, Baptisti, Presbiteri, sijaribu kuyabomoa madhehebu ya—ya—yao, ninajaribu tu... Kaa kwenye lolote ulilomo, hiyo ni sawa, kwa sababu, nitawaambia hili, hakutakuwa na shirika lolote *fulani* litakalowakilishwa katika Siku hiyo, itakuwa tu ni watu binafsi kutoka kwa dhehebu hilo. Mnaona? Na dhehebu ni kitu tu ambacho—ambacho ni makubaliano madogo tu kati ya ndugu wanaoona hivyo, nao wanakwenda hivyo. Sasa, hilo ni sawa.

20 Kwa mfano, labda watu wawili wanaofanana kabisa wanapaswa kuwa ni mtu na mkewe. Nina mwanamke mzuri zaidi duniani. Sasa, najua ninyi ndugu hamtakubaliana nami, namna hiyo, lakini—lakini na—nafikiri ninaye, kwangu mimi ndivyo alivyo. Mnaona? Lakini hata hivyo, tunapokula sambusa, yeye atachukua sambusa ya tofaa, nami nitachukua cheri, yeye ni mke wangu hata hivyo. Naam, bwana.

21 Na kwa hiyo, mvulana wangu, Billy Paul, mnajua hadithi ya maisha yangu, mama yake alikufa alipokuwa na umri wa miezi kumi na minane, dada yake mdogo alikuwa na umri wa miezi minane nilipowazika pamoja. Nilimbeba Billy kote na ninii yangu...chupa yake mfukoni mwangu, nikitembea sakafuni, nikilia pamoja naye, akimlilia mamaye, nami sikuwa na mama wa kumpa. Nimekuwa wote wawili baba na mama kwake, hiyo ndiyo sababu ninamweka papa hapa pamoja nami sasa, popote twendapo mimi humchukua Billy, nilimwahidi hivyo alipokuwa akifa. Hakuna mtu aliye karibu sana kuliko mimi na Billy.

22 Nanyi, mwajua, magari yetu yote mawili yalikuwa yamechakaa. Ilitubidi sote wawili kununua magari mapya kabla ya kuja huku, na huwezi kuniuzia lolote ila Ford, na ni hivyo tu, wala huwezi kumwuzia lolote ila Chevy, lakini sote tulifika hapa. Breki zangu ziliungua, nayo redieta yake ikachemka kote kote, lakini hatukuwa tukitumainia magari yetu, tulikuwa tukimtumainia Mungu, hiyo ndiyo sababu tumekuja hapa. Kwa hiyo, mnaona, hicho ni kitu kama dhehebu.

23 Ninataka ndugu wote waliofadhili, walioko mkutanoni, wasimame, tafadhali, kwa muda kidogo tu. Ndugu waliokuwa wafadhili wa huu mkutano, simameni tu, ninyi ndugu wahudumu wote, ambao wamekuwa...[Ndugu mmoja anasema, "Ndugu, tungewafanya tu wote wasimame."—Mh.] Wa—wahudumu wote wasimame, hata uwe wapi. Kwangu mimi...Hebu endeleeni tu kusimama kwa muda kidogo, tafadhali, ndugu. Hilo ni sawa.

24 Kwangu mimi, waliochaguliwa, wakatengwa kwa wadhifa fulani, labda wahudumu hao...Kamwe huninii...Kamwe sipendi kumdhalilisha mchungaji mbele ya watu wake, kwa sababu hata hivyo, amewekwa kama mchungaji. Wachungaji wenu hapa huenda wasiweze kupambanua roho na kutabiri mambo yatakayotukia, huenda wasiweze kufanya hivyo, lakini

wana mahali, wala mimi si mwalimu, wala mimi si—si mtume. Mnaona? Ofisi hizi tano . . . Na kila mmoja wa hao watu ana ofisi, naye ameshikilia ofisi yake, na ofisi hiyo ni kubwa tu machoni pa Mungu kama ofisi nyingine yoyote.

25 Nami nataka mjue jambo hili, ya kwamba mimi kukuombea halingemaanisha zaidi ya mmoja wao kukuombea. Si lazima ungoje hadi Ndugu Roberts, Ndugu Allen, au—au baadhi ya hawa ndugu wengine waje kukuombea, mchungaji wenu ana haki ile ile niliyo nayo, ama mtu yeyote aliyo nayo. Kweli. Wao ni watu wa Mungu, na Mungu amewaita kwenye ofisi yao.

26 Sasa, sisi hapa tumesimama alasiri ya leo, labda wa baina ya madhehebu, Utakatifu wa Kipentekoste, na Assemblies of God, Foursquare, na Open Bible, wote walio pale, tunasimama tofauti, lakini sisi sote ni watoto Wake, sisi sote ni watumishi Wake.

27 Sikilizeni, jambo moja tu kabla hamjaketi. Nina watoto watano, na ninapoenda kununua aiskrimu, sijawahi kuona mkusanyiko kama huo! Mmoja anataka chokoleti, mwingine anataka vanila, mwingine anataka ndizi-chungwa, na mwingine anataka, ama, chungwa, na rangi zote mbalimbali. Ninaporudi na aiskrimu, ni kama upinde wa mvua, sijawahi kuona rangi nyingi hivyo, lakini hebu niwaambie, zote ni aiskrimu, nao hao wanaokula ni watoto wangu; hivyo ndivyo ilivyo alasiri ya leo.

28 Mnajua, ladha haijalishi katika hili. Tunaweza kutofautiana katika shirika, dhehebu, lakini Mungu ni Mungu wa aina mbalimbali, Mungu anapenda aina mbalimbali, Yeye si Sears and Roebuck Harmony House. Mungu ni wa aina mbalimbali, ana milima mikubwa, milima midogo, maua meupe, maua ya waridi, maua ya manjano. Yeye ni Mungu wa aina mbalimbali, ana watu wadogo, watu wakubwa; anao wenye nywele nyeusi, nywele nyekundu, za shaba, na aina zote mbalimbali. Ana majangwa, ana—ana maziwa, ana bahari. Mnaona? Yeye ni Mungu wa aina mbalimbali.

29 Na hivyo ndivyo ilivyo hapa leo, sisi sote ni watumishi wa Mungu. Na hata hivyo, ndugu, hivi yote ni . . . ? Upinde wa mvua unawakilisha agano. Hiyo ni kweli. Tuko katika agano la Mungu. Hiyo ni kweli. Pamoja, kama ndugu, tunasimama. Bwana awabariki, ndugu zangu wema, na makanisa yenu na yakue na kufanikiwa, na Mungu awabariki sana daima na kwa wingi ndilo ninii langu—ndilo ombi langu aminifu. Ikiwa ninaweza kuwa wa msaada kwenu kwa njia yoyote, usiku hauingii giza sana, wala mvua hainyeshi kwa nguvu sana, niiteni tu, nitafanya kila niwezalo kuwasaidia.

30 Tunafanyia kazi Ufalme mmoja mkuu: wa Mungu. Hiyo ni kweli. Na tuseme mmoja ni wa Assembly, labda hiyo ndiyo ladha yake, huyo mwingine ni wa Open Bible, hiyo ndiyo ladha yake, bali wote ni Ufalme wa Mungu. Hiyo ni kweli. Popote tulipo, wote ni Ufalme wa Mungu ndio tunaofanyia kazi. Unashuka,

"Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," nasi tunakuwa viungo vya Kristo.

31 Nataka kuwashukuru, enyi ndugu, katikati ya migogoro kuendelea kunifadhili kuja hapa, kunileta mbele ya watu wenu. Nisingemdhuru mtu bure, ni kondoo wenu, Mungu aliwapa muwalee.

32 Kwa kawaida siku ya mwisho, ninge-. . . nilikuwa nikiwaambia watu waniandikie maswali, wayaweke kwenye jukwaa langu. Mnaona, ikiwa mna—mna maswali, najua mnayo, lakini mwulizeni mchungaji wenu, yeye ndiye anayeweza kuwaambia. Mnaona? Sikutumwa kujibu maswali, ninalihubiri tu hivi na kuendelea. Mnaona? Kuja tu kwa. . .

33 Sisi sote ni wavuvi. Je, mlijua hilo? Ufalme wa Mungu ni kama mtu aliyechukua wavu na kwenda baharini. Nami naja kuunganisha wavu wangu na nyavu zao, kufanya mrusho mkubwa wa wavu mjini kote, kuvuta ndani. Wengine wameingia, sijui wao ni nini. Mtu anapoingiza wavu ndani, ana samaki mla mizoga, ana kasa, kamba, lakini ana samaki pia; ni kazi ya Mungu kujua gani ndiyo gani. Na kwa hiyo, baadhi yao watabakia, baadhi yao hawatabakia, hatujui, hiyo ni juu ya Mungu. Inatubidi tu kuvuta wavu ndani, naye Baba anachukua yeyote a—aliye—aliyemchagua kuwa hivyo. Nami. . . nini. . . Kumbukeni, wakati wavu ulipowashika, haidhuru walikuwa kitendo cha aina gani, walikuwa samaki wa aina hiyo hapo mwanzo. Mnaona?

34 Na kwa hivyo, hatujui kuna samaki wangapi ziwani bado, hatuna budi kuwavua mpaka tuwatoe wote, na ndipo Yesu atakuja. Na kwa maoni yangu, marafiki, tunashuka sana, nafikiri tumezama sana, ndugu. Ni vigumu sana, tena (Mnajua hilo, katika makanisa yenu.), kupata watu wanaotaka kumtumikia Kristo kwa dhati, ni vigumu sana, sana.

35 Sasa, Bwana na awabariki. Nami nawatakeni. . . Samahani sarufi yangu, baadhi ya matamshi yangu fidhuli. Sijui, sina elimu, kwa hiyo inanibidi tu nitegemee uvuvio, hivyo basi mimi tu. . . kila njia ninayoipata tu. Nimekuwa nikiwaweka kwa muda mrefu, lakini ninaifikia tu na kuinyakua, na kuitema jinsi ninavyoipata. Kwa hiyo hilo ni fidhuli, lakini hiyo ndiyo njia pekee niliyo nayo ya kulifanya. Kwa hivyo ninyi tu. . . Ninajaribu tu kufika hapa na kuanza kuzungumza, kidogo, mpaka nipate upako, ndipo nikipata upako, ninaondoka tu.

36 Ni wangapi waliowahi kuwinda sungura? Umewahi kutumia mbwa mwindaji? Atanusia kote, akiinua kinywa chake, mwajua, mpaka aipate njia yake. Anapopata harufu hiyo ya sungura, jamani, anakodoa macho yake, na masikio yake yanainuka, naye huyo anaenda. Uh-huh. Hivyo ndivyo mhudumu anavyowinda somo lake, anapojaribu kuhubiri kwa uvuvio (Je, hilo si ni ufidhuli?), mpaka atakapoanza.

37 Inanikumbusha, nina wasichana wawili wachanga. Miaka mingi iliyopita, walikuwa jamaa wadogo. Wao ni...Mmoja wao ni karibu mwanamke kijana sasa, Rebekah, lakini yeye amemzidi Sarah kwa miaka minne, halafu nikampata mtoto Joseph. Kama ninyi nyote mjuavyo, Bwana alinionyesha yeye akija miaka sita kabla hajaja, mnakumbuka habari zake. Na kisha...Lakini wasichana hawa wawili...Hii, ni kabla Joseph hajafika hapa. Kwa hiyo kuna tofauti ya miaka minne kati ya Sarah, Rebekah, na kwa hiyo, wote wawili ni wasichana wa Baba, ninawapenda watoto wangu, nafikiri kila mtu ni vile vile. Kuna kitu kuhusu upendo wa hao jamaa wadogo!

38 Na hivyo, wangeninii...Ilinibidi...Nilikuja kutoka mkutanoni. Na kwa hiyo, Mama alikuwa...Hao wasichana walingojea, lakini ndege haikufika kwa wakati, ndipo mchanga ukawaingia hao wasichana wadogo machoni mwao, bila shaka, mwajua, ikabidi walale. Kwa hiyo Mama akangoja hadi karibu saa nane usiku, ndipo hatimaye nikaja, nami nilikuwa nimechoka sana.

39 Hivyo ndivyo nilivyo sasa. Nimeninii tu...Ninapaswa kupumzika. Mimi...Huu ni mkutano wangu wa nane mfululizo, nina mingine mitatu kabla sijapumzika. Na kisha ninaninii...

40 Nilikuwa nikiwazia, nilipokuja asubuhi hiyo, nilikuwa nimechoka sana nisingeweza kulala, nikajilaza chini kwa muda kidogo, nikarudi sebuleni na kuketi ki—kitini. Nami nilipokuwa nimeketi pale kukapambazuka, nami nilikuwa nikiwasikiliza ndege wakianza kuimba huko nje. Ndipo kitambo kidogo nikasikia kitu kikipinduka, huko kwenye chumba cha watoto, basi ilikuwa—ilikuwa ni Rebekah, alikuwa ameamka. Ndipo akakumbuka, "Kumepambazuka, Baba anapaswa kuwako!" Huyu hapa anakuja, haraka tu alivyoweza.

41 Vema, alipotambaa akatoka, alimwamsha Sarah, dada yake mdogo. Na Becky kidogo ni mwembamba, na macho makubwa ya shaba, ya samawati; Sarah ni mfupi, nywele nyeusi, macho ya kahawia, kama mama yake. Kwa hiyo hapa, akamwamsha Sarah.

42 Na mimi sininii...Nadhani watoto wenu pia, wao... tunavaa nguo za kupokezana, mwajua, nyumbani kwangu. Kwa hiyo Sarah alikuwa amevaa pajama za Becky, naye alivaa zilizokuwa na miguu mirefu sana, mwajua, basi maskini jamaa huyo mdogo asingeweza kuendelea vizuri sana, akipitia nyumbani nazo, miguu mikubwa ya sungura ikipeperuka, mwajua, huku akijaribu kumpita Becky awe wa kwanza kunifikia, lakini Becky akamshinda.

43 Kidogo inanikumbusha juu ya kanisa ambalo limekuwako, mwajua, muda mrefu, kanisa la kale, limekuwa likiendelea huko nyuma kabisa, dhehebu kubwa, huko nyuma kabisa, na maskini dhehebu dogo, jipya la Pentekoste.

44 Mnajua, jambo la kwanza lilikuwa, Becky aliingia mbio na kuruka pajani mwangu, na kunikumbatia kwa mikono yote miwili namna *hiyo*. Basi wakati maskini Sarah alipofika pale, hiyo miguu mikubwa ikikokotwa sakafuni huku amevaa pajama za Becky, aligeuka akamwangalia Sarah, akasema, "Sarah, dada yangu, nataka ujue kitu," akasema, "Nilikuwa hapa kwanza." Hiyo ndiyo wanayojaribu kutuambia, ndugu, walikuwa hapa kwanza. "Nilikuwa hapa kwanza," huku amenikumbatia kwa mikono yote miwili, kisha akasema, "Ninaye Baba wote, wala hakuna kilichosalia kwako."

45 Maskini Sarah, aliinamisha mdomo wake mdogo chini, macho yake madogo ya hudhurungi yakageuka rangi, nikachomoa mguu wangu *hivyo*, na kuinua kidole changu, na kumwashiria, hivyo ndivyo tu ilivyonipasa kufanya, huyu hapa akaja akiipeperusha hiyo miguu mikubwa kama ya sungura, akaruka juu ya paja langu. Nami nikachukua . . .

46 Kidogo alikuwa mchanga, mwajua, mwajua, hakuwa amekuwako huku muda mrefu sana, naye ana miguu mifupi, wala asingeweza kufikia sakafu, kwa hiyo akaanza kuyumbayumba, kwa hiyo nikamkumbatia kwa mikono yote miwili kumshikilia. Mnaona, hakuwa thabiti kama Becky alivyokuwa, Becky alikuwa amekaa muda mrefu zaidi kidogo, angeweza kuweka miguu yake sakafuni, alikuwa amekuwepo kwa muda mrefu zaidi, lakini Sarah kidogo alikuwa mchanga, mwajua, kidogo anayumbayumba, kama Kanisa sasa, kwa hiyo hakuwa amekaa sana. Kwa hiyo nikamshika kwa mikono yote miwili, asianguke, nilifikiri angeanguka, sakafuni, alikuwa ni jamaa mdogo, nami nikamvuta karibu nami.

47 Akastarehe kifuani mwangu, sitasahau hili, akageuza macho hayo makubwa ya hudhurungi, akamwangalia Becky, akasema, "Rebekah, dada yangu, nataka kukwambia jambo fulani." Akasema, "Huenda ikawa kwamba unaye Baba wote, lakini nataka ujue jambo moja, Baba ana mimi wote."

48 Hivyo ndivyo ilivyo, huenda nisiyatamke maneno yangu vizuri, huenda tusitamke vizuri, ndugu, lakini jambo moja, maadamu tu Yeye ana sisi sote! Kwa hivyo hata hatuzingatii kile tunachofanya, tunaendelea tu kukisema. Hiyo ni kweli. Hebu awe na sisi sote. Hiyo ni kweli.

49 Nafikiri shida na huduma yetu ya Kipentekoste, ni kwamba tunaninii . . . tumeona mengi sana mpaka yamekuwa ya kawaida kwetu. Sidhani kama tunatha-. . . Mimi, samahani, hebu nirekebishe hilo, sikumaanisha kusema mimi . . . hatulithamini.

50 Lakini mimi . . . Kama vile kulikuwa na—na methali ya kale huko Uingereza, nami niliisikia mara moja, kwamba m—mshairi alikuwa akiandika mashairi mengi, naye alikuwa hajawahi kuiona bahari, kwa hivyo siku moja akawazia, atashuka aende baharini. Basi alipokuwa njiani akishuka, akakutana na mzee

mwanamaji (ninyi watu mnajua, wanayemwita baharia mzee.) na, akitoka baharini na kiko chake kinywani mwake, na—na masharubu kwenye kidevu chake, na yapata umri wa miaka sitini. Ba—ba—basi yule kijana mshairi alikuwa akishuka kwa mikogo, ndipo huyo mzee baharia akamwambia huyo kijana mshairi, akasema, "Unakwenda wapi, mtu wangu mwema?"

51 Akasema, "Ee bwana," akasema, "Mimi ni mshairi," kisha kasema, "Nimeandika juu ya bahari, na. . .lakini sijawahi kuiona bado, basi ninashuka huko." Kasema, "Loo, siwezi kungoja hadi nione bahari, kuwasikia shakwe, nikatazame anga angavu za samawati zikijiakisi katika ninii wake—katika mkusanyiko wake mkubwa wa maji, niyanuse maji ya chumvi, na kuona hayo mawimbi meupe yakinyunyizia *hivyo*!"

52 Huyo mzee baharia akatoa kiko chake, akatema mate, akasema, "Huh. Sioni kitu cha kusisimua hapo, nimekuwa huko kwa miaka sitini." Mnaona? Hiyo ni kweli. Alikuwa juu yake sana, ilikuwa ni kawaida kwake. Mnaona?

53 Hiyo ndiyo shida ya Kanisa. Tumeuona wema wa Mungu sana hata umekuwa wa kawaida kwetu. Hiyo ni kweli, ndugu, dada. Hiyo ni kweli.

54 Inanikumbusha hadithi ndogo niliyosikia mwaka jana, duka la bei rahisi huko Louisville, kulikuwa na mama mmoja aliyekuja mle ndani, naye alikuwa na mtoto mchanga yapata, alionekana kuwa na umri wa miezi miwili hivi, ama, umri wa miaka miwili, mvulana mdogo. Naye alikuwa akizunguka kwenye vipambo vidogo vyote, mwajua, ambavyo wanawake, jinsi nyinyi wanawake mnavyopenda kununua katika maduka ya bei rahisi, kama vile mke wangu. Sikuzote anapoenda katikati ya mji, nawasikitikia watu wanaohudumu kwenye hilo duka la bei rahisi, yeye kamwe hanunui chochote, huenda tu na kukiangalia, anakiweka chini. Na yeye na binti-mkwe wangu walikuwa huko chini, loo, jamani, jamani!

Na kwa hivyo, angechukua kitu, aangalie, "Naam, angalia hapa. Unaonaje juu ya hiki?"

"Uh-huh."

Mama huyo angesema, "Unataka chochote?"

"La, mama. La mama."

55 Anakirudisha, anakitupa chini mahali fulani, na kuchukua kitu kingine, na kisha hana budi kuja moja kwa moja kukiweka vizuri. Vema, nadhani hiyo inaburudisha, kwa hiyo sawa. Kwa hiyo ni sawa. Hilo ni zuri na safi. Endelea tu kulifanya, mradi tu unafanya hivyo, basi hiyo ingekuwa sawa. Mnaona? Kwa hiyo usilifanye baya zaidi.

Kwa hiyo basi, mwanamke huyu alikuwa na mvulana huyu mdogo, naye angembeba kote, anachukua kipambo kidogo na kusema, "Angalia, Mpenzi. Angalia, angalia."

56 Naye akaendelea tu kukodoa macho moja kwa moja mbele yake. Ndipo akaenda kwenye kaunta nyingine, naye akachua kitu kingine, na vitu vidogo ambavyo vingemvutia mvulana mdogo wa umri huo, na—naye mvulana huyo mdogo akakodoa macho tu moja kwa moja mbele yake, huku amekodoa macho yake. Basi hatimaye, wateja wakaanza kuona matendo yasiyo ya kawaida ya huyo mwanamke.

57 Na kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo akaangukia tu moja ya hizo kaunta na kuanza kupiga mayowe. Ndipo wateja wakamkimbilia huyo mama kuona ni nini. Akaendelea kusema, "La, la. Hiyo, sivyo."

Nao wakasema, "Kitu gani sivyo?"

Kasema, "Yeye . . . Ndio kwanza tutoke kwa daktari. Huyo daktari anasema amepata nafuu, bali hajapata."

Naye huyo mteja akasema, mmoja wao akasema, "Naam, Mama, kuna—kuna nini?"

58 Akasema, "Hivi majuzi, alianza tu kukodoa macho angani. Yeye . . . Kitu chochote kinachopaswa kumvutia mvulana mdogo wa umri wake, hakimvutii." Kasema, "Nimetikisa kengele ndogo na kila kitu ambacho kinapaswa kumvutia, wala havimvutii, anakodoa tu macho angani."

59 Sasa, nashangaa . . . Sasa, hebu niseme hivi, kwa utamu niwezavyo. Sijui kama Mungu hajatikisa kila karama ndogo ambayo angeweza mbele ya Kanisa ambayo inapaswa kulivutia Kanisa lililozaliwa mara ya pili, na bado tungali tunakodoa macho tu angani na hatuonekani kutambua ya kwamba ni Mungu akituonya juu ya siku hii ya mwisho tunayoishi. Hebu tukumbuke jambo hilo, rafiki.

60 Mungu amemtikisa Oral Roberts, na mimi . . . chochote, mambo ya kila namna mbele ya watu. Na, bila shaka, tunajua Shetani ametikisa vitu pia, lakini wewe dumu na Maandiko, nawe utajua ni lipi la Mungu na ni lipi lisilo. Unaona? Lakini mambo haya yote ambayo Mungu amefanya . . . Wakati Shetani anatikisa kitu *hapa* kukuondoa njiani, wewe dumu moja kwa moja na Maandiko. Tuangalie Mungu anafanya nini.

61 Sasa, ningependa kusoma Maandiko fulani. Mkitaka . . . Na sasa, leo nilikuwa nikitaka kuhubiri juu ya somo nililokuwa nalo, sijawahi kuhubiri juu yake bado, nimejaribu pwani yote, wala sijaligusia bado. Lakini nilipanda pwani wakati huu, kwa sababu, kama nilivyosema jana usiku, ninaamini yale mawimbi makubwa yanasonga huku na kuipiga pwani, kuna—kuna pazia hapa, hayawezi kwenda mbali zaidi, ni pazia la Mungu la wakati.

62 Kwa kuwa mnazungumza juu ya mapazia, hebu niwaonye, kitu fulani. Mmesikia juu ya pazia la chuma, sivyo? lile pazia la mwanzi la mashariki? Kunalo, ila kuna mapazia matatu. Sasa, hebu niseme hili ili liweze . . . lisidhuru, lakini mtajua

ninachomaanisha. Kuna pazia lingine, linaitwa pazia la zambarau; angalieni hilo. Hilo ndilo mliangalie, litachukua mamlaka, lakini iweni waangalifu. Mnaona? Litakuwa danganyifu sana, lingewadanganya walio wateule kama yamkini. Mnaona?

63 Na kila mtu anaogopa ukomunisti. Hakuna Andiko katika Biblia, linalosema jambo lolote kuhusu ukomunisti, ila tu kwamba u—utamtetekeza yule kahaba kwa moto. Unatumika moja kwa moja mikononi mwa Mungu, lakini ninyi uangalieni Urumi, hicho ndicho kitu kitakachofanya hivyo. Ninyi angalieni tu. Sio huo . . . Mpinga Kristo si mtu wa namna hiyo ambaye anakataa kila kitu katakata, unafanana sana hata utawadanganya walio wateule kama yamkini, Yesu alisema. Ninyi uangalieni huo, hicho ndicho kitu mnachoweka akilini mwenu.

64 Sasa, na huku na huku pwani, ninajaribu kupanda kila Mbegu niwezayo, kuvuta kila kitu ninachojua jinsi ya kuvuta kwa Ufalme wa Mungu.

65 Nawashukuru nyote tena. Niliwauliza ndugu kama walilipia gharama zote, nao walizilipia, nami nashukuru kwa hilo. Walisema walichukua sadaka ya upendo, nitaiweka hiyo moja kwa moja katika misheni katika nchi za ng'ambo. Mimi mwenyewe situmii pesa, ninapata mshahara kidogo kutoka kanisani mwangu, dola mia moja kwa juma, na hiyo tu ndiyo mimi . . . hizo ndizo ninazopata. Vinginevyo, pesa zozote zinazochukuliwa huenda kwa misheni za nchi za kigeni, nami ninaenda kule mwenyewe na kuwahubiria makafiri Ujumbe ule ule ambao nyote mnausikia hapa. Nami—nami najaribu kufanya vizuri zaidi, kwa sababu najua sina budi kuwajibika kwa pesa mnazonipa.

66 Na kwa matoleo yangu mwenyewe, sikuwahi kuchukua sadaka maishani mwangu. Nimekuwa nikihubiri miaka thelathini na mmoja, nina umri wa miaka hamsini na mitatu, na kamwe sijachukua sadaka maishani mwangu. Na kamwe hatuji . . . kwa ajili ya matoleo na kadhalika, lakini sikuzote nimewaambia ndugu, iwapo hawawezi kugharamia matumizi, mnijulishe, maskani huko Jeffersonville itayasimamia. Mnaona? Kwa hiyo hatutaki kamwe . . . Hatuko hapa kwa ajili ya umaarufu, hatuko hapa bure ila kuwasaidia. Nasi tunatumaini kwamba tumekuwa wa msaada kidogo kwenu, na bila shaka mmekuwa kwetu.

67 Na halafu, alasiri ya leo, nilikuwa ninaenda kuhubiri juu ya somo: *Wakati Mashariki Na Magharibi Zinapokutana.* Nilikuwa ninaenda kuliweka, labda wakati mmoja nitaliweka, wakati nikilijengea msingi, kama nifanyavyo kila wakati, mpaka nifike kwenye mstari wa kuendea, ambapo walipigilia msumari huo wa dhahabu, wakati ya asili, na, mashariki

na magharibi zilipokutana, lakini sasa, upande wa kiroho umekutana, Mungu ameteremsha msumari wa dhahabu pia. Labda, wakati mwingine . . .

68 Lakini ni . . . Niliahidi kuwaombea wagonjwa jana usiku. Niliuliza, na kulikuwa na kundi kubwa la watu waliotaka kuombewa. Kwa hiyo hebu tuchukue ninii cha watoto . . . ni chakula cha watoto. Na leo hii nataka kuchukua somo linalojulikana kidogo, nilizungumzie kwa dakika ishirini zijazo, Bwana akipenda, ishirini na tano, thelathini tukiendelea sana, ili niweze kuharakisha, kwa sababu Billy aliniambia ya kwamba alishuka na kusambaza kadi nyingi za maombi.

69 Ni wangapi hapa walio na kadi za maombi kuombewa? Naam, ni kila mahali. Mnaona? Na itakuwa ninii kubwa . . . Na ni wangapi hapa ambao hawana kadi za maombi na bado wanataka kuombewa? Tutajaribu kuwafikia pia, kwa hiyo, tuone ya kwamba kila mtu ameombewa. Nami nitafanya kila niwezalo.

70 Nami nataka kusema hivi, kuna mara nyingi ambapo nimetazama maono juu ya watu, hakuna kitu asichoweza kutujulisha, lakini mnaona, ono halikuponyi. Mnajua hivyo. Ono . . . Mnasema, "Vema, tunaona . . . "

71 Sasa, mtu fulani alisema . . . aliniandikia barua miaka michache iliyopita, na kusema, "Ilimbidi Mungu kumwinua Oral Roberts kuwaombea watoto Wake wagonjwa." Kasema, "Oral Roberts atawaombea mia tano kabla hujawaombea wawili." Vema, pengine hiyo ni kweli. Lakini, mnaona, Mungu alimpa Oral Roberts huduma naye anafanya yale ambayo Mungu anamwambia afanye, kisha akanipa moja, nafanya yale anayoniambia nifanye. Huduma zetu ni tofauti. Huduma yangu . . . Ya Oral ni ile ya kuwawekea mikono. Oral ana imani ile ya jibwa-kali kuinuka pale na . . . Lakini mimi, mimi humchunguza mtu huyo kwanza.

72 Hebu niwaulizeni jambo fulani. Vipi kama ugonjwa huo ni wa kusudi hilo . . . mtu huyo kwa kusudi fulani? Je, mwajua, unaweza kupata shida nyingi kumwondolea mtu huyu kitu ambacho Mungu ameweka hapo?

73 Mnajua, nabii husimama mahali pa hatari. Mnajua, Musa alijiweka nje ya nchi ya ahadi kwa kufanya kile hasa Mungu alimwambia asifanye, akiwasikiliza watu. Je, mliwahi kuwazia hilo?

74 Je, mliwahi kuwazia ilikuwa ni mapenzi ya Mungu wakati Eliya, yule nabii mashuhuri, mwenye upara, nao maskini watoto hao wadogo walimkimbilia huko chini wakimdhihaki kwamba ana upara? Naam, vipi basi? Alipaswa tu kuliachilia, lakini chini ya hasira, basi nabii huyo akageuka na kuwalaani watoto hao, nao dubu wawili wa kike wakawaua watoto arobaini na wawili, nabii mwenye hasira. Hiyo ni kweli?

75 Unapaswa kuwa mwangalifu sana, sana. Hiyo ndiyo sababu karama hazitumwi jinsi watu wanavyodhania hutumwa. Karama za kweli za Mungu hutumwa kutoka kwa Mungu, nanyi mnaziangalia. Jukwaani, angalieni muone.

76 Huyu hapa mwanamke, labda, amesimama hapa, tatizo dogo tu la kike. Vema, vipi ikiwa amefanya jambo fulani *hapa* ambalo limesababisha hilo? Litaendelea kuwa mbaya zaidi mpaka hilo . . .

77 Sasa, tuseme, huyu hapa mwanamke amelala hapa, amesimama hapa, ama amelala hapa kwenye machela labda, ama mwanamume, labda mtu huyo ni—ni mtu aliyekosa maadili, lakini amelala hapo akiwa na yabisi-kavu. Bila shaka, sijawahi kumwomba Mungu kwa dhati pasipo yeye kuitimiza, ama labda kuniambia kwa nini hangeweza, na hiyo ni kweli kabisa.

78 Nikimtazama mtu huyo naona ana ugonjwa wa yabisi kavu, lakini hapo amefanya jambo baya. Sasa, vipi kama nikichukua imani yangu hii ya mbwa kali, kama ni—kama nilikuwa nayo, sina, lakini kama ningekuwa nayo, na kukimbia kule na kumvuta mtu huyo, na kumfanya atembee, halafu, ile laana ya Mungu imewekwa juu yake, nami niiondoe kwa karama? Nina shida na Mungu.

79 Hiyo ndiyo sababu katika mstari wa maombi, ninaangalia kwa makini sana na kuona kile anachoniambia. Na kama nikiendelea kusema nao, nami naona inaendelea kumulika, kumulika, kadhalika, nuru, Nikiona hakuna kosa, basi nina haki ya kuja, unayo haki ya kuja.

80 Lakini unaweza kummiminia mwanamume au mwanamke mafuta siku nzima, na kuruka-ruka, na kupiga kelele kwa sauti yako yote, na kuwalaani pepo, atakaa pale pale, kwa sababu ana haki ya kukaa pale, dhambi isiyoungamwa na kila kitu. Mnaona? Kwa hiyo, mnaona?

81 Lakini kuna hamsini wanaoponywa katika mkutano wa Ndugu Roberts kwa mmoja katika wangu, lakini kwa kawaida, wangu ni wale ambao walishindwa katika yake. Mnaona? Wao huja hapa, ndipo ujue shida iko wapi, halafu inanyooshwa, na kisha mambo yanarekebishwa. Mnaona? Ni wangapi wameona hilo likitukia katika mikutano yangu, yeyote? Mbona, hakika. Bila shaka. Mnaona? Hakika. Mnaona?

82 Kwa hiyo ni—ni pole pole, kuchukua muda, kuangalia, kuwa na uhakika ya kwamba uko sahihi, ndipo unaweka laana hiyo juu ya ibilisi, basi kama mtu huyo ataamini nusu, litatendeka. Naam, bwana. Haidhuru linachukua muda gani, kaa nalo; limesemwa, kaa nalo. Mungu hutoa ahadi, na wakati mwingine ni—ni majuma na miezi kabla haijatukia, bali haina budi kutukia kama huitilii shaka, haina budi kutukia, ni imani yako katika yale uliyoona yakifanywa.

83 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena. Ninii tu... Mtu fulani aliniambia nina makosa mawili makuu, mojawapo, kujivunia sana Yesu; na jambo lingine ni kuwa mara nyingi sana katika maombi, siwezi kufanya hilo kupita kiasi, "Ningependa watu waombe kila mahali." Ninapenda kuzungumza Naye. Nami ninacho kilichonunuliwa na Damu Yake hapa mikononi mwangu alasiri ya leo, sina budi kufanya vizuri zaidi niwezavyo.

84 Baba wa Mbinguni, niongoze sasa, na hili kanisa dogo, hapa, linaniombea, nisaidie, tumia midomo ya mtumishi Wako. Na tena, tunaomba ya kwamba watakumbuka kwamba juma hili katika ibada, kila usiku, umekuwa hapa, umejithibitisha Mwenyewe hapa, hiyo ndiyo sababu nimekuwa nikijaribu kuwafanya, Bwana, wajue tu ya kwamba ni Wewe. Pasipo kuwagusa, hakuna njia hata kidogo, kwa hiyo wasingeweza kusema ya kwamba ilikuwa ni mikono yangu, Bwana, lakini ni imani yao wenyewe katika mikono hiyo yenye makovu ya misumari, Yule tunayempenda sana, sio kuweka mikono yangu, bali imani yao kukugusa Wewe. Lakini leo, Bwana, tutawaleta katika mstari wa maombi, ninaomba ya kwamba utampa kila mmoja wao imani.

85 Na sasa, nimechagua Maandiko madogo hapa, Maandiko yanayojulikana kidogo ya kuzungumzia, kujenga imani ya watu, sio kuzungumzia hali za wakati, kama ambavyo nimekuwa nikifanya, ama kwenye ujumbe fulani wa kinabii, bali kuhusu uponyaji wa Kiungu. Kwa kuwa sisi...Inawabidi wawe wanawazia hilo kusudi Roho Mtakatifu afanye kazi juu yao. Sasa, tujalie, Bwana.

86 Tusaidie sasa, Uwepo Wako na uje katikati yetu, na jalia kuwe na mtetemeko mkubwa hapa, alasiri ya leo, ili tukienda kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia tuseme, kama wale waliotoka Emau siku ile, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, alipokuwa akisema nasi njiani?" Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi wote mikononi Mwako sasa, mimi mwenyewe.

87 Kama nilivyosema kitambo kidogo kilichopita, huenda tusikutane tena hapa, wazee wengine wako hapa, vijana wengine watakuwa wametuacha; ninaweza kuwa nimeenda mwenyewe hivi karibuni, sijui. Hatujui. Lakini labda, kama nikirudi baada ya mwaka mmoja, wengi hawangekuwa hapa, ama, wako wengine.

88 Na, Baba, ninaomba ya kwamba utatusamehe dhambi zetu zote, na kuelekeza nyuso zetu Kalvari pamoja na wanaume na wanawake waaminifu mbele za Mungu. Tubariki sasa Neno linapotokea, na ulilete katika Jina la Yesu. Amina.

89 Huko katika Maandiko, ninawatakeni msome katika Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 12, na ninataka kuanzia kifungu cha 38:

Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakisema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta *ishara; wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona:*

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Na *watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki, nao watakihukumu: kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.*

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

90 Kama ningelichukua kama somo, kwa, labda kwa njia tofauti, ningesema hivi: *Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Wote Yupo Hapa.*

91 Yesu alikuwa akikikemea kizazi hicho kwa sababu kilishindwa kumtambua. Sasa, nawatakeni msikilize kwa makini. Na sababu ya mimi kubadilisha somo langu kutoka *Mashariki na Magharibi Kukutana* kuwa hili, ilikuwa ni kwa sababu ku—kujenga imani kwenye Kristo Mponyaji, badala ya Kristo Mwokozi, Kristo Mponyaji, Mtu yule yule, lakini, ili imani ye—yenu itakuwa ikitazamia uponyaji, kwa sababu huo ndio tulioutengea siku hii, kuwaombea wagonjwa.

92 Sasa, kile kizazi alichokuwa akizungumza nacho, alikuwa akiwakemea. Ukisoma hu—huo mlango, vema, mwa—mwanzoni mwa huo mlango, tutaona kwamba Yesu alikuwa akitenda kazi Za—Zake. Alikuwa mwonaji, hakuwa tu mwonaji, alikuwa Mungu na mwonaji. Alikuwa nabii, hakika.

93 Walimwuliza Yohana Mbatizaji, "Je, wewe ni Eliya? Je, wewe ni Musa? Je, wewe ni Yeremia? Je, wewe ndiye *yule* Nabii?" Mnaona? "Je, wewe ndiye *yule* Nabii ajaye?"

94 Ni nani *huyo* Nabii? Ikiwa unayo Biblia ya Scofield, au— au Mfululizo wa Thompson, au yoyote unayotaka, chukua maandishi yako ya pambizoni, yatarejesha kwa Masihi, kwa sababu Masihi angekuwa huyo Nabii mkuu. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Semeni, "Amina." Yeye alipaswa kuwa Nabii *huyo*, na ndivyo aliyokuwa. "Je, wewe ndiye Nabii *yule* ajaye?" ikimaanisha Masihi.

95 Hiyo ndiyo sababu yule mwanamke kisimani akamwambia, "Huna budi kuwa nabii. Naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua

ya kwamba Masihi, atakapokuja, atatwambia mambo haya." Mnaona? Alikuwa akimtazamia huyo Nabii-Masihi.

96 Naye Yesu, kama tulivyokuwa naye katika somo letu jana usiku, *Sauti Isiyojulikana*, basi, tunaona kwamba—kwamba wengi walikuwa hawajafunzwa kwa Sauti hiyo ya Neno, nao wakalikosa Neno lilipotoa sauti, kwa maana Yeye alikuwa Neno. Hebu tuseme hilo pamoja. "Yeye alikuwa Neno." Sasa, hebu tuliseme tena. "Yeye *ni* Neno. Yeye *ni* Neno." Hiyo ni kweli.

97 Na yote aliyokuwa Mungu, ambayo yalikuwa ni Neno, aliyamimina ndani ya Mwanawe, ndipo Mwanawe akawa Mungu Neno. Na yote aliyokuwa Mwana, alitoa uhai Wake, Mungu akauinua huo mwili, maskani, ameketi mkono Wake wa kuume, na yote yaliyokuwa ndani ya Mwana, ambayo yalikuwa ni Baba, aliyamimina ndani ya Kanisa katika Jina la Roho Mtakatifu. Kwa hiyo ilikuwa ni Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Mnaona?

98 Kwa hiyo ikiwa uhai wa kitu chochote uko ndani ya kitu kingine, kinafanya kazi zake. Kwa mfano, vipi kama ningewaambia uhai wa John Dillinger ulikuwa ndani yangu? Whiu! Ungekimbia na kujificha. Ningekuwa na bunduki kubwa na kuwa mhalifu, kwa sababu uhai wake uko ndani yangu. Ningekuwa hatari kusimama mbele yangu. Vema, vipi kama ningewaambia uhai wa msanii fulani mkuu, mashuhuri ulikuwa ndani yangu? Mngetarajia nichukue bra—bra—bra—brashi ya kutia rangi alasiri hii, na kuweka kipande cha turubai hapa, na kuyashika hayo mawimbi ya kupendeza ya chumvi, niliyozungumzia, yule mshairi, ama misonobari hii mirefu ya kupendeza, na kuipaka rangi hapo mpaka ikaonekana kana kwamba wewe ulikuwa umesimama pamoja nayo. Ikiwa roho yake ilikuwa ndani yangu, ningeweza kufanya hivyo.

99 Vema basi, ikiwa Roho wa Mungu yuko ndani ya mtu, atafanya kazi za Mungu. Yesu alisema vivyo hivyo, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Mnaona?

100 Na jinsi watu walivyokuwa wameenda kombo kwenye kanuni za imani na kadhalika! Naye Yesu akawaambia, akasema, "Mmezichukua amri za Mungu, na kuzitangua kwa mapokeo yenu." Na kisha wanasema, "Mungu yuko wapi? Ilikukwaje kwa Mungu wa Musa?" Mungu wa kihistoria ana faida gani ikiwa Yeye si Mungu yeye yule leo? Mnaona?

Inafaa nini kulisha kurumbizi wako vitamini nzuri za kila namna, na kutengeneza mifupa mikubwa yenye nguvu, na manyoya mazuri, kisha kumweka kizimbani?

101 Ina faida gani kusoma historia ya Biblia, na kujifunza juu ya Mungu mkuu aliyefungua Bahari ya Shamu, Mungu aliyeshusha mapigo, Mungu aliyetambua mawazo yaliyokuwa katika nia za watu, Mungu ambaye angeweza kuwaponya

wagonjwa, na kusema, “Loo, lakini siku za miujiza zimepita”? Inaleta faida gani ya kuwasomesha watoto wetu katika mambo kama hayo, kama tuna—kama tuna—kama tunaninii . . . ? Ni jambo la kusikitisha.

102 Siku moja nilikuwa huko Cincinnati, Ohio, nami nikamchukua mtoto Sarah, ambaye nilikuwa nikizungumza habari zake dakika chache zilizopita, na wakati Mama alikuwa akiandaa chakula cha jioni kwenye meza ya mandari kule, tulishuka kwenda kutazama mbuga ya wanyama, ninii . . . ndipo nikasikia kelele, nami nikaenda kule, na kulikuwako na tai mkubwa, nao ndio kwanza wamkamate na kumweka kwenye kizimba hiki.

103 Nami nina heshima kubwa sana kwa tai. Ninyi nyote mmesikia mahubiri yangu, *Kama Tai Ataharikishavyo Kiota Chake*. Nami sikuzote nilimwangalia tai, kwa maana Mungu aliufananisha urithi Wake na tai, naye Mwenyewe ni Yehova-Tai, kwa sababu tai anaweza kuruka juu kuliko ndege mwingine yeyote. Kwani, kama mwewe angejaribu kumfuata, angesambaratika! Halafu basi, inamfaa nini kufika huko juu ikiwa hana jicho la kuona atakapofika huko? Yeye ni ndege aliyejengwa maalum. Mungu anawafananisha manabii Wake na tai, wanapaa juu sana, wanaweza kuona mambo kabla hayajafika huku. Mnaona?

104 Sasa, nami nikamwangalia tai huyo, jamaa huyo mkubwa mno, nilimhurumia sana, a—alikuwa amelala pale kichalichali, akafingirisha macho yake makubwa ya mahameli, akitazama huku na huku. Akaamka, akarudi nyuma *hivi*, nami nikaona kichwa chake kinavuja damu, nikaona mabawa yake yanavuja damu, naye angeangalia *kule* juu mawinguni, juu ya kizimba, naye angerudi apate kuanza kuondoka, naye huyu hapa angekuja, naye angegonga hicho kizimba kwa kichwa chake huku hayo mabawa makubwa yanapapatika, manyoya yanang’oka, damu inaruka kutoka kichwani mwake namna *hiyo*, naye angeanguka kichalichali kwa kichwa chake na kutazama *kule* juu.

105 Mnaona, yeye ni ndege wa mbinguni, alijengwa kwa ajili ya mbingu, alijengwa apate kupaa juu, lakini mafanikio ya mwanadamu yalikuwa yamemnasa. Huyo hapo jamaa huyo, angeweza kuangalia nje, na angeweza kuona makazi yake, lakini kitu fulani kilikuwa kimemfungia ndani ya kizimba.

106 Niliwazia hiyo ilikuwa ndiyo ninii zaidi . . . Ningeliwapa hao kila senti ya pesa niliyokuwa nayo wakamfungulie. Lakini nini? Alikuwa amenaswa na hila za mwanadamu, amenaswa. Hata angeweza kuona anga, naye aliundwa kwa ajili ya hizo, lakini asingeweza kuzifikia, alikuwa akiligongesha bongo lake tu.

107 Nikawazia, “Hilo ndilo jambo la kusikitisha zaidi ambalo nimewahi kuona.” Lakini basi niligeuka, machozi machoni

mwangu, kisha nikaenda kule, na kumweka mtoto Sarah mapajani mwangu, nami nikasema, "Angalia, Kipenzi. Unaona hilo?" Ndipo Kitu fulani kikanijia, kikasema, "Hilo silo la kusikitisha kuliko yote, Ndugu." Hebu niwaambieni. Vipi kuhusu wanaume na wanawake ambao wamezaliwa kuwa wana na binti za Mungu, wanaoweza kuangalia katika Biblia hii na kumwona Mungu anayeweza kukomboa, na kufanya kila namna ya miujiza mikuu na kadhalika, halafu kizimba fulani cha kikanisa, kinawafungia ndani? Nanyi mnaweza kuangalia huko nje na kuona kwamba kweli huko ndiko . . . Kitu fulani ndani yako kinavuta nje.

108 Lakini cha kikanisa kinasema, "La, usifanye hivyo, huo—huo ni ulokole. Usiamini hilo." Loo, ndugu, usikae umefungiwa kwenye kizimba namna hiyo. Kuna Mtu aliyekuja siku moja ambaye aliilipa hiyo gharama, upate kutoka humo: Yesu Kristo. Unapoona kazi Zake zikiendelea, udhihirisho Wake, nguvu Zake, wewe amini kwamba, ni kwa ajili yako. Amini tu kwa moyo wako wote, kwa sababu ni kwa ajili yako pia, "Yeyote atakaye."

109 Na kulikuwa na Mtu mwema ambaye alipitia hapo siku moja, na kukununua, akalipa gharama na kukutoa kwenye kizimba hicho. Ukitaka kutoka, mlango uko wazi, na yuko Mtu, amesimama mlangoni na mikono inayovuja damu, anakuashiria kwa mkono, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

110 Na wakati Wayahudi hao, ambao—ambao walidhani na kukiri kwamba walimjua Mungu, na kisha wakaona Neno lile lile la Mungu likidhihirishwa, na bado wanaliita kazi ya ibilisi!

111 Mama aliyeketi nyuma *kule* jana usiku, hakujua alikuwa akizungumza na binti-mkwe wangu, alisema, "Huyo jamaa ni bandia." Natumaini hilo litaingia ndani yako vizuri, Mama. Hebu njoo hapa jukwaani, usimame hapa, kama ukiondoka ukiwa hai, basi mimi ni bandia. Sasa, njoo huku. Ikiwa mimi ni bandia, acha nife nikiwa nimesimama hapa mbele zenu. [Ndugu Branham anatulia—Mh.] Una akili kuliko nilivyodhania. Hata hivyo, turudi kwenye somo langu. Sio bandia! Unafikiri ungeweza kuyaficha hayo mawazo? Usingeweza hata ufanyeje.

112 Ufuasi wa kanisa haufanyi chochote. Usiutumainie huo, afadhali ukimbilie Kalvari.

113 Sasa, Yesu alikuwa akikemea kizazi hicho. Alikuwa amefanya mambo haya, akasema, "Yachunguzeni Maandiko. Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Si Mimi ninayefanya hivyo, ni Mungu, Neno ndani Yangu likijidhihirisha Lenyewe." Yeye alisema, "Kama sizitendi kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama ninazifanya hizo kazi, hata hivyo hamniamini Mimi kama Mwanadamu . . . "

"Je, anawezaje kuwa mwanadamu na kuwa Mungu?" Wasingeweza kuelewa.

114 Kasema, “Ikiwa hilo ni fumbo kubwa sana kwenu, basi aminini tu kazi nizifanyazo. Hamwezi kuzielewa, aminini tu kazi hizo, angalieni kama ni za Kimaandiko.”

115 Wala hakufanya jambo moja ila lililokuwa la Kimaandiko, wala Yeye kamwe hakufanya jambo moja mpaka Mungu alipomwonyesha, katika ono, la kufanya, la sivyo alisema uwongo katika Yohana 5:19, alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha. Mnaona? Lakini yale Baba aliyomwonyesha yalikuwa katika Maandiko kikamilifu, kulingana na Maandiko. Naye alisema, “Ni nani kati yenu anayeweza kunishtaki Mimi kwamba nina dhambi?”

116 Hapa si muda mrefu uliopita, rabi mmoja . . . John Rhyn aliponywa, kipofu kabisa, hakuninii . . . alikuwa ombaomba, akiuza penseli huko Fort Wayne kwa takriban miaka ishirini, kipofu kabisa, nao wakamleta mkutanoni, alikuwa Mkatoliki, naye akapanda jukwaani, ndipo akasema . . . akaja, na kulikuwa na mwanamke aliyepitia jukwaani. Bwana alikuwa amemponya mwanamke huyo mwenye tezi kubwa shingoni, kabla hajafika pale, akarudi mbio akipiga kelele, akionyesha shingo yake, hakuwa nayo.

John Rhyn ndiye aliyefuata, alikuwa akisikiliza hilo. Nami nikamwangalia, nikasema, “Bwana, wewe ni Mkatoliki kwa—kwa dini.”

Naye akasema, “Hiyo ni kweli.”

Kisha nikasema, “Umekuwa kipofu kwa muda gani?”

Akasema, “Miaka ishirini *na kitu*, Bwana.” Kasema, “Nilikuwa nikisafiri na ‘Garland’ katika Barnum na Bailey, nilikuwa mcheshi.”

Nikasema, “Sawa.”

117 Nasi tukaanza kuongea hapo kwa dakika chache, nikamwangalia, nikaona huyo mzee alikuwa mwaminifu. Nikamwona amefumbuliwa macho, anaona, nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, upate kuona.”

Sasa, angalieni. Sasa, usiruke haraka sana anapokuambia chochote, hiyo ni wewe unayefanya hivyo, basi ngojea uone kile Yeye anachosema baadaye. Unaona?

Basi mzee huyo, walichukua . . . Wote wakaanza kulia. Wakamwondosha jukwaani. Na katika dakika chache tu, huyu hapa amerudi mstarini tena.

Akasema . . . Nilimwuliza kwanza, nikasema, “Je, unaniamini mimi ni mtumishi Wake?”

Akasema, “Naam, bwana.”

Nikasema, “Mimi ni mgeni kwako?” Akasema . . . Mnajua jinsi ninavyofanya kwa kawaida, ninawasiliana na roho yake wakati huo.

Akasema, “Naam, hiyo ni kweli.”

118 Nikasema, “Ikiwa Bwana anaweza kunifunulia jambo fulani, utaninii . . . ulichofanya, au ulilopaswa kufanya, au kile unachotaka,” na kadhalika. Ndipo akarudi nyuma, na kumwambia mambo haya yote mbalimbali, halafu baada ya hayo, likaja ono, nikamwona, naye alikuwa ameponywa, nami nikamwambia ya kwamba alikuwa ameponywa.

119 Akarudi mstarini, wakamrudisha tena, na kwa hiyo, wakamtoa mstarini kule chini, hakuninii . . . tayari ameachilia kadi yake ya maombi. Kwa hiyo basi nami nikauliza kuna nini.

Akasema, “Bwana, uliniambia nimepona.”

Nikasema, “Wewe uliniambia uliniamini.”

Akasema, “Nakuamini.”

120 Nikasema, “Unaniuliza maswali ya nini basi? Sio mimi niliyekwambia, uliponywa, ilikuwa ni ‘BWANA ASEMA HIVI,’ Hiyo haikusema, ‘Ninasema hivyo,’ Yeye Ndiye aliyekuwa anazungumza. Yule Yule anayeweza kukuweka chini ya uvuvio, anaweza kukwambia yale ambayo yamekuwa, kisha akuweke chini ya uvuvio apate kukwambia kitakachokuwa. Ukijua kama ‘yamekuwa’ yalikuwa ni kweli au la, hakika ungeweza kuamini ‘yatakuwa.’”

Akasema, “Sielewi.”

Maskini huyo jamaa, alilelewa katika kanisa Katoliki, ha—hakuelewa chochote kuhusu mambo ya kimbinguni. Nami nikamwambia . . .

121 Kulikuwa na msichana mdogo wa Kiamishi wakati huo, mmeisikia hiyo hadithi, aliruka kutoka kwenye piano, alikuwa akicheza *Ni Tabibu Wa Karibu,* akaruka na kuanza kupiga mayowe, nywele zake zilianguka chini ya mwili wa—wake namna *hiyo*, kisha akaanza kupiga kelele, nayo piano ikaendelea kucheza, “Ni Tabibu Wa Karibu, Yesu mwenye huruma,” halafu akisimama pale, alikuwa akimtukuza Mungu.

Nami nikasema, “Jambo unalopaswa kufanya, ni kuendelea kumsifu Mungu kwa uponyaji wako.”

122 Kasema, “Vema, Bwana. Asante, nimefurahi kujua hilo.” Sasa, Wakatoliki wamefundishwa kuamini kile asemacho kasisi wao kwamba ni kweli. Hivyo alikuwa . . . Nilikuwa nikitenda kama tu kasisi kwake.

123 Kwa hiyo kesho yake usiku alikuwa mkutanoni, alikuwa amerudi huko juu kwenye roshani ya pili, naye angesema, mara moja moja, kasema, “Kila mtu atulie. Mungu asifiwe kwa kuniponya!” Vema, alikuwa akifuata maagizo. Kwa hiyo baadhi ya mabawabu, wakienda kupanda juu, kumfanya atulie, nikasema, “Msifanye hivyo. Mwacheni.”

Na kwa hiyo, kote mtaani, kila mahali alipoenda, alikuwa akisimama mara moja moja, "Mungu asifiwe kwa kuniponya!"

124 Kwa hivyo alikuwa akiuza magazeti pembeni. Yapata majuma mawili au matatu baada ya kanisa . . . baada ya ibada kwisha, bado alikuwa amesimama kule chini, angepaza sauti, "Ziada! Ziada! Mungu asifiwe kwa kuniponya! Ziada! Ziada! Mungu asifiwe kwa kuniponya!" Nao watu wangemcheka tu, kila mtu, alikuwa tu ni kitu cha kuchekesha.

125 Kwa hiyo kulikuwa na maskini mwanahabari mwingine aliyekuja, nao wakampeleka kwa kinyozi akanyolewe. Alitaka kuvuka kule, naye huyo mvulana mdogo akamwongoza kuvuka barabara. Akajilaza kitini, ndipo kinyozi, mmoja wa maskini hao *wajuaji*, mwajua, na hivyo akaupaka uso wake sabuni, na kunoa wembe wake, kisha akaanza kunyoa nusu ya uso wake chini.

Akasema, "Aisee, Dadi Rhyn."

Akasema, "Naam, Bwana. Ni kitu gani, Mwanangu?"

Kasema, "Nilisikia ulikuwa hapa juu kumsikiliza mhubiri yule mtakatifu anayejibingirisha alipokuwa hapa juu."

Kasema, "Naam, nilikuwa huko juu."

Akasema, "Nilisikia ati uliponywa."

126 Akasema, "Naam. Mungu asifiwe kwa kuniponya!" Ndipo macho yake yakafungukia kwenye hicho kiti cha kinyozi. Huyo akatoka kwenye kiti hicho, akaenda mbio barabarani akiwa amejifunga taulo shingoni, huku kinyozi akimfuata. Onyesho kubwa sana hujawahi kuliona! Naye mtu huyo anahubiri Injili leo hii. Amina. Kwa nini? Aliamini Neno la Mungu. Naam, bwana.

127 Niliitwa huko Benton Harbor, Michigan. Kuna rabi, shule hiyo, shule ya Kiyahudi huko, niliitwa kule kwa mahojiano na rabi huyu, jamaa mdogo, ndevu nyekundu na nywele nyeusi. Naye . . . Nilikuwa nikingoja pembeni pamoja na Bw. Rhyn, akaja, akasema, "Jina lako ni nani?"

Nikasema, "Jina langu ni Branham."

"Um-hum." Naye akasema, "Bw. Branham, ningependa kukuuliza swali."

Nikasema, "Naam, bwana."

128 Akasema, "Ulifungua macho ya John kwa njia gani?" Akasema, "Ninajua John amekuwa kipofu, ninampa sadaka mara nyingi." Kasema, "Ulifungua jicho lake kwa njia gani?"

Nikasema, "Katika Jina la Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo."

Akageuza kichwa chake na kuangalia pande zote kidogo, akasema, "Yeye si Bwana na Mwokozi."

Nami nikasema, “Vema, labda sio kwako, lakini ndivyo alivyo kwangu mimi.” Naye akasema . . . Nikasema, “Yeye ndiye Masihi.”

Naye akasema, “Hakuna Masihi.” Kasema, “Mwizi angewezaje kuwa Masihi?”

Nikasema, “Ati mwizi? Unamaanisha nini, Rabi?”

Akasema, “Naam, alikuwa mwizi.” Nikasema . . . Kasema, “Maandiko yenu wenyewe yalisema alikuwa mwizi.”

Nikasema, “Loo, unasoma kitu ambacho si sahihi, hakiko katika Biblia.”

“Naam,” akasema, “nitalithibitisha. Alipitia kwenye mashamba ya mahindi siku ya Sabato na kuiba mahindi.”

Nikasema, “Hapana, alivunja masuke. Unaona?”

129 Naye akasema—akasema, “Naam, alichukua kitu ambacho hakikuwa chake. Huyo si angekuwa ni mwizi ikiwa ulichukua kitu ambacho si chako?”

130 Nikasema, “Rabi, unataka kuniambia kuwa hujui sheria zenu za Walawi? Hakuvunja sheria yoyote, sheria ya Mungu. Sheria inasema kwamba unaweza kupita shambani na ule, lakini usiweke chochote mfukoni na kukitoa nje.” Sheria yake mwenyewe! Hiyo ikamshinda.

Akasema, “Niambie, ulimfanyia nini John Rhyn?”

Nikasema, “Sikufanya lolote, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyafungua macho yake.”

“Yeye si Mwana wa Mungu.”

Nikasema, “Kwa nini siye?”

Akasema, “Ninyi Mataifa hamwezi kumkatakata Mungu vipande vitatu na kumpa Myahudi.”

Nami nikasema, “Vema, hatumkati katika vipande vitatu.”

Akasema, “Aw, hakika mnajaribu kufanya hivyo.”

Nami nikasema, “Rabi, unaamini manabii wenu?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Isaya 9:6 ilisema nini?”

“Kwetu amezaliwa Mwana.”

Nikasema, “Alikuwa akizungumza juu ya nani?”

Kasema, “Masihi.”

Nikasema, “Basi Masihi atakuwa nini?”

Kasema, “Masihi atakuwa Mungu.”

131 Nikasema, “Niambie ni wapi Yesu alishindwa kuthibitisha kwamba hakuwa Huyo?” Hilo lilimshika. Nilimwona akiwa amesimama pale kwa dakika chache. Nikasema, “Kuna jambo moja la hakika: Wewe unajua kwamba John alikuwa

kipofu, unajua sasa anaona. Nami nikasema kwamba hakuna kitu ningeweza kufanya, ila ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Masihi wenu wenyewe mliyemkataa, kama baba zenu walivyofanya, ndivyo na ninyi, Rabi."

132 Katika dakika chache, akasema, "Kama ningehubiri upuuzi kama huo, ningeninii . . . " Tulikuwa . . . shule ilikuwa hapa juu ya kilima, ikielekea ziwani, kasema, "Ningekuwa huko chini, nikiomba-omba huko chini barabarani."

133 Nikasema, "Rabi, ni afadhali nihubiri ukweli, na niwe huko chini, nimelala kifudifudi, nikinywa maji ya chumvi na mikate mikavu, kuliko kuwa na kuku wa kukaanga mara tatu kwa siku, na jina langu katika dhahabu kwenye jengo hili hapa juu, huku nikijua nilikuwa makosani." Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

Alipoanza kuondoka, machozi makubwa yalikuwa yakidondoka ndevuni mwake, akaanza kutembea, naye akasema, "Nitakuona wakati mwingine."

Nikasema, "Ngoja kidogo, Rabi."

Akasema, "Nitakuona baadaye." Asingezungumza nami.

134 Ndivyo hivyo. Alidumu na Neno. Haidhuru Yeye alifanya nini, alikuwa angali katika Neno, kwa maana Yeye alikuwa Neno. Ndipo watu hao hawakumwamini, na kumwambia Yeye alikuwa Beelzebuli, ibilisi, kila namna ya maneno maovu.

135 Vema, kama angeingia Kanisani leo, asiyeamini angesema jambo lile lile, kwa hiyo mnaona linakotoka. Na wale watu waliosema kwamba walikuwa watu watakatifu, wakitenda utakatifu, waliishi safi, na walikuwa waaminifu. Uaminifu sio, "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu," mnaona, "lakini mwisho wake ni njia za mauti."

136 Kwa hiyo Yesu alikuwa amesimama pale akiwakemea kwa kumwita Beelzebuli. Aliyatambua mawazo yao, hawakusema kwa sauti kubwa, alitambua mawazo yao, Naye akasema . . . akawaambia kuhusu hilo. Ndipo wakamwendea, baada ya yote aliyokuwa amefanya, na kuwaonyesha ishara sahihi ya Masihi, na kazi zikaifuata, yale hasa yalisemekana angefanya, ndipo wakapanda juu, na kusema, "Bwana, sisi tungetaka kuona ishara kwako." Loo, jamani!

137 Sasa, chukueni hili katika upendo wa Kikristo, chukueni hili kutoka katika moyo uliojaa upendo kwenu, lakini ninii tu . . . ni kurudiwa. Tungetakaje kufanyiza mstari wa maombi, upitie hapa, mkutano mwingine, wakati tulisimama papa hapa na kuona Biblia ikidhihirishwa na Uwepo wa Yesu Kristo papa hapa miongoni mwetu? Mtazamo Wake kwa mmoja ni kwa wote. Mnaona? "Lakini tungetaka kuona ishara kutoka kwako." Ishara hiyo ilifanywa wakati mmoja, na mji wote wa Sikari ukamwamini Yesu Kristo, lakini hawakuiona ikifanywa, waliamini ushuhuda wa yule mwanamke, naye

alikuwa kahaba, wakati mmoja, na maelfu ya wakati imefanywa kote ulimwenguni sasa, iangalieni.

138 Lakini mnajua, wakati Yohana alipokuja kumwandalia Yesu Kanisa, hakukuwako na mmoja katika milioni moja ya watu waliowahi kumsikia. Na wakati Yesu Kristo alipokuwa duniani, hapakuwa na mmoja kati ya laki moja ya watu waliopata kumwona au kumsikia (Lakini alikuja kwa wale waliokusudiwa Uzima, nao wakaupokea.) na wale aliowachagua, Yeye alichukua tu mia na ishirini kutoka kwao. Mnaona?

139 Kuna watu wachache tu watakaoupokea, na ni hivyo tu, hivyo tu. Hao wengine, unaweza kuwamwagilia maji na namna zote za kila kitu, kamwe haitaleta—haitaleta kamwe u—ukweli mbele, haitauamini kamwe. Mnaona? Itaendelea tu mbele, maana hakuna kitu ndani yake cha kuaminia. Kama maskini mama yangu mkusini alivyozoea kusema, "Huwezi kupata damu kutoka kwa mboga nyekundu," kwa sababu hakuna yoyote ndani yake.

140 Sasa, "Tungetaka kuona ishara." Yesu akawakemea. Sasa, tunajua ya kwamba Mungu, katika nyakati zote, amekuwa na ishara yenye karama. Hakujapata kuwa na wakati ambapo Mungu hakuwa na aina fulani ya ishara akijidhihirisha Mwenyewe mahali fulani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .-nahistoria yeyote kati yao anaweza kuwaambia hilo, kwamba nyakati zote, Mungu daima amekuwa na ishara Yake. Ametoa ishara katika nyakati zote.

141 Halafu, Yesu alizirejea, Naye akasema, "Kizazi kiovu, au, kizazi dhaifu na cha zinaa hutafuta ishara." Sasa, hebu nipate jambo hilo kwa karibu. Si—sitaki kuchelewa sana sasa, nina kama matamshi manne au matano tofauti hapa ya kutoa, nami nitayataja haraka iwezekanavyo ili tuanzishe mstari, lakini nataka mhakikishe kuwa mmelipata. Angalieni, "Kizazi dhaifu na cha zinaa hutafuta ishara."

142 Tunajua kanisa la Korintho, sikuzote ilimbidi Paulo kuwaambia. . .Mmoja alikuwa na zaburi, na mmoja alikuwa na lugha, na mmoja alikuwa na *hii*, na mmoja alikuwa na *ile*. Mbona kama. . .Paulo aliamini katika kunena kwa lugha, lakini hakuwaambia Waefeso. Angeweza kuwafundisha kuchaguliwa tangu zamani na mambo makuu, lakini watoto hawa wachanga, ilimbidi kuwapa chakula cha watoto bado, mnaona, asingeweza kusimama na kuwaambia mambo ya juu.

143 Nao ulimwengu umejaa Ukorintho siku hizi. Hakika. Mungu ni Mungu mwema, atafanya hivyo ili kuwaonyesha. Lakini. . . Yeye ni Mungu mwema. Kama vile Tomaso alivyosema, "Bwana, kabla sijaamini kuwa ni Wewe, itanibidi kutia mkono wangu katika makovu Ya—Yako ya misumari, na ubavuni Mwako."

144 Yeye ni Mungu mwema, akasema, "Njoo hapa, Tomaso." Kasema, "Sasa, umeona na kusadiki. Je, ni kubwa jinsi

gani thawabu yao ambao hawajawahi kuona na hata hivyo wanasadiki!" Mnaona, mnaona? Amini kwa sababu Neno lilisema hivyo.

145 Ni thawabu kubwa jinsi gani mji wa Sikari utapokea kuliko Yerusalemu katika Siku ya Hukumu, mnaona, kwa sababu waliamini wala hawakuona, walisikia tu na kuamini, maana walikuwa wakiitazamia!

146 Sasa, Yeye alisema, "Lakini watakuwa kizazi kiovu na cha zinaa." Sasa, kama nilivyosema jana usiku, na sote tunajua, kwamba kila unabii una maana maradufu, maradufu, unajirudia.

147 Je, mliwahi kusoma pale katika Mathayo 3 ambapo ilisema, "Kutoka Misri nimemwita Mwanangu, ili litimie . . ." Yesu alipokwenda Misri? Chunguza marejeo yako pale, uone kama haimaanishi Yakobo, lakini Yakobo alikuwa mwanawe, na vivyo hivyo Yesu alikuwa Mwanawe. Mnaona, ina . . . kila wakati inajirudia, kama historia. Neno la Mungu ni la Milele, linaendelea tu.

148 Sasa, angalieni, Yeye alikuwa anazungumza juu ya kizazi kiovu na cha zinaa. Hebu niseme jambo hili kwa unyofu, alikuwa akizungumza juu ya kizazi hiki. Kwa maana kama kuliwahi kuwa na kizazi dhaifu, kinachokera, kilichojaa uzinzi kama taifa hili, watu hawa!

149 Angalieni, taifa letu linaongoza ulimwenguni kwa talaka. Ushoga ni mbaya kuliko ulivyo huko Paris, Ufaransa. Nilisoma makala, hivi majuzi, ambapo asilimia arobaini ya wafanyakazi wa serikali waliwaziwa kuwa ni mashoga. Nilikuwa nikiruka juu ya Los Angeles hivi majuzi, na yakawekwa gazetini katika jimbo la Los An- . . . la California pekee, mashoga, mwaka mmoja kabla ya ule uliopita, waliongezeka kwa asilimia ishirini.

150 Ofisi yangu imejaa barua za akina mama wakilia, wavulana wao wakiwachukua wavulana wengine na kuingia vyumbani na kuishi nao. Wamejitumia vibaya sana, na kadhalika, mpaka wamepotosha njia ya asili kati ya mwanamume na mwanamke.

151 "Kizazi dhaifu na cha zinaa chatafuta ishara," kizazi hiki, kinachoangalia, nao wataipokea. Kitu gani? Ishara ya Yona. Kitu gani? Watapokea ishara ya ufufuo. "Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa ndani ya tumbo la nyangumi siku tatu usiku na mchana; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi," lakini atafufuka tena. Nacho kizazi kiovu na cha zinaa kitapokea ishara ya ufufuo. Mnalipata?

152 Sikuzote nilimhurumia Yona. Watu wengi sana walisema ya kwamba Yona, alirudi nyuma. Siamini hivyo, ninaamini kama alikuwa nabii, Neno la Mungu lilikuwa pamoja naye katika kila . . . Mungu hupanga hatua za wenye haki. Hamwamini hilo?

153 Sasa, tunajua alipaswa kwenda Ninawi, ule mji mkuu, uliojaa dhambi na uzinzi, nao ukaja mbele za Mungu, na, kundi la Mataifa kule chini. Lakini angalieni, jiji hilo lilikuwa karibu ukubwa wa St. Louis, kubwa mara kadhaa kuliko mji huu hapa, nao walikuwa waovu tu. Naye alipaswa kushuka kule, bali akakata tikiti yake kwenda Tarshishi, ninaamini hayo yalikuwa ni mapenzi ya Mungu. Angalieni, akaingia baharini, ndipo dhoruba ikatokea, nao wakaifunga mikono yake wakamtupa baharini.

154 Hapa si muda mrefu uliopita huko Louisville, Kentucky, walikuwa na fremu ya nyangumi imewekwa juu ya—juu ya (Loo, imekuwa kama miaka kumi na mitano, ishirini iliyopita, nadhani.), imewekwa kwenye be—behewa kubwa, naye yule jamaa aliyesimama pale nje akasema, "Sasa nataka kuwaambia, mmesikia hiyo—hiyo hadithi ya kubuni kuhusu Yona kumezwa na nyangumi." Akasema, "Ninataka kuwaonyesha jinsi hiyo isivyowezekana." Kasema, "Mtu asingeweza kupitia kwenye koo la nyangumi huyu." Loo, alikuwa wa kisayansi kwelikweli, mwajua.

Akasema, "Mnaona, ingekuwa vigumu kwa besiboli kupitia kwenye koo lake." Naye nyangumi huyu alikuwa na uzito, nasahau wa tani ngapi.

Nilisimama tu kadri niwezavyo, hivyo nikasema, "Bwana, naweza kusema neno?"

Kasema, "Ni nini, Kijana Mwanamume?"

155 Nikasema, "Unashindwa kuelewa Neno la Mungu. Mungu kamwe hakusema alikuwa nyangumi, alikuwa ni samaki maalum. Mungu alimweka tayari samaki, huyu angemeza nyumba kama angelitaka." Hiyo iliyapunguza manyoya yake. Mnaona? Huyu alikuwa samaki maalum, "Mungu alimwekea tayari samaki." Alikuwa na koo kubwa, naye alikuwa amemmeza mhubiri huyu, nayo mikono yake ilikuwa imefungwa, miguu yake imefungwa.

156 Na, mwajua, unapomlisha samaki wako wa dhahabu, unajua kinachotokea? Mbona, anaenda moja kwa moja . . . Baada ya kuzunguka-zunguka majini kutafuta chakula chake, ndipo akilijaza tumbo lake, anashuka moja kwa moja chini kabisa ya huo mtungi mdogo wa samaki wa dhahabu, na kupumzisha maskini pezi zake chini, na kupumzika. Hivyo ndivyo afanyavyo, samaki wote hufanya hivyo.

157 Basi samaki huyu mkubwa maalum hapana shaka alifanya vivyo hivyo. Huenda ikawa . . . Sijui ilikuwa na kina cha mita ngapi huko nje, lakini alizunguka-zunguka mpaka akammeza Yona, halafu hapana shaka alishuka chini kabisa na kupumzisha pezi zake kule chini kabisa, akiwa amelala mle. Huyu hapa Yona, chini katika tumbo la nyangumi akipinduka katika matapiko.

158 Mnanena . . . nyie watu hunena kuhusu dalili, alikuwa na kisa chake. Baadhi yao huombewa, kasema, "Mnajua, mimi—mimi . . . mkono wangu sio bora zaidi." Hiyo ina uhusiano gani nao? Nilifikiri uliamini. Mnaona? Kasema, "Ni—ni—ni—ni—ni—ni—ni—ningali ninaumwa na kichwa." Hiyo ina uhusiano gani nao? Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, kama unayo robo inayonunua mkate, mkate hauna budi kuja, unaona, una gharama ya bei yake.

159 Naye huyu hapa Yona, kama kuna mtu aliyekuwa na haki ya kuwa na dalili, yeye alikuwa nayo. Angalieni, kama aliangalia *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, akiangalia *kule*, tumbo la nyangumi, *huku* kulikuwa ni tumbo la nyangumi; kila mahali alipotazama palikuwa ni tumbo la nyangumi, na mikono yake ilikuwa imefungwa na miguu yake ilikuwa imefungwa, naye alikuwa chini ya bahari katika tumbo la nyangumi kwenye siku yenye dhoruba. Nena kuhusu dalili! Hakuna mtu katika hali hiyo mbaya hapa, nina hakika. Naye huyo hapo amelala. Lakini mnajua alichosema? Alisema, "Ni ubatili wa uongo, sitaamini sehemu yake yoyote. Lakini mara nyingine tena nitalikabili hekalu Lako takatifu."

160 Alijua wakati Sulemani alipoweka wakfu hekalu hilo, aliomba dua, na kusema, "Mungu, ikiwa watu wako watakuwa katika shida popote pale na kulikabili hekalu hili takatifu, basi sikia kutoka Mbinguni," naye akaamini.

161 Ndipo Mungu, sijui alichofanya, akaweka mtungi wa oksijeni au kitu fulani mle chini na kumdumisha hai kwa siku tatu mchana na usiku, kwa sababu alilikabili hekalu ambalo Sulemani aliliweka wakfu, na baadaye akarudi nyuma, lakini alikuwa chini ya uvuvio alipokuwa akiomba, naye Mungu akayaheshimu maombi hayo na kumdumisha hai kwa siku tatu mchana na usiku.

162 Ikiwa Mungu angeyaheshimu maombi yake kwa dalili za aina hiyo, anapaswa kutufanyia nini siku hizi? Wakati watu wanaponywa kila mahali kote karibu nasi, nasi haitulazimu kuangalia kwenye hekalu lililojengwa kwa mikono ya wanadamu, bali Hekalu la Mungu ambamo Yesu ameketi mkono wa kuume, pamoja na Damu Yake Mwenyewe, haleluya, Hekalu ambalo haliwezi kufifia, tunapaswa kufanya nini basi? Amina. Shikilia hilo, endelea mbele.

163 Mnajua, hao watu, kule chini Ninawi, walikuwa makafiri. Waliabudu kila aina ya miungu wa kipagani, naye mungu wa bahari alikuwa nyangumi, bila shaka. Kama vile Wahindi hapa walivyokuwa wakimwabudu dubu mkubwa mkali, alikuwa ndiye mtawala wa misitu, Wapekowisi.

164 Hivyo basi, wakati hao—wakati hao . . . Mungu mkuu wa bahari alikuwa ni nyangumi, na kazi yao ilikuwa ni wavuvi. Na hapa wote, katika asubuhi hii yenye joto la jua angavu, kila mtu

alikuwa huko nje akitupa nyavu zake, maelfu juu chini ukingoni wakitupa nyavu zao, huyu hapa mungu wa baharini anakuja, kila mtu akasimama kuabudu, akautandaza ulimi wake, nabii akatoka moja kwa moja kinywani mwake.

165 Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo. Hakika wangemsikiliza, mungu wao akamtema nabii ukingoni. Mnaona, hakuna kitu kinachoenda vibaya, Mungu hufanya kila kitu kifanye kazi sawa. Basi akahubiri, naye Mungu akayaheshimu maombi yake. Hakika. Si ajabu Yeye alizungumza kuhusu kizazi cha Sulemani, au—au, kizazi cha Yona. Ishara ya ufufuo.

166 Kisha, upesi sasa katika kufunga. Alimtaja Malkia wa Kusini, katika siku za Sulemani. Sasa, kila mtu anajua ya kwamba Mungu anapotuma karama duniani, nayo ikikataliwa, ni mchafuko kwa kizazi hicho. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika mnajua. Na kama wakipokea karama hiyo, ni enzi ya ufanisi kwao.

167 Loo, jinsi walivyompokea Sulemani na karama yake! Kila mtu, moyo mmoja na nia moja. Mbona, ilienea ulimwenguni kote! Ni wakati mzuri jinsi gani! Kila mtu: "Laiti ungaliona huko Israeli, wanaye mtu kule, walimfanya mfalme wao. Loo, Roho wa Mungu wao yuko moja kwa moja ndani ya huyo mtu! Mbona, ana karama ya upambanuzi! Hujawahi kuona kitu kama hicho. Ni kamilifu." Ni mazungumzo ya namna gani!

168 Ingekuwa ni mazungumzo ya namna gani siku hizi kama taifa hili lililorudi nyuma lingemrudia Mungu na kukubali Karama Yake, Roho Mtakatifu ambaye ametumwa kwake! Urusi ingekoma kutengeneza makombora ya atomiki, silaha za nyuklia. Ndiyo ngome bora zaidi tunayoweza kuwa nayo, ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia akirudi katika taifa hili.

169 Ingefunga kila nyumba ya kahaba, ingefanya mwuzaji pombe haramu kukauka sana, ingembidi kujikakamua kwa dakika kumi na tano apate unyevu wa kutosha kutema mate. Ingeninii—ingeninii, kabisa, ingetufanyia jambo fulani, kama tu tungeiruhusu ifanye. Hiyo ni kweli. Hiyo, ingefunga kila kilabu cha pombe, na kila karamu ya roki ingefungwa, nayo mikutano ya maombi ingekuwa kila mahali, badala ya makelele haya yote ya upuuzi wanayopiga siku hizi. Naam, bwana. Ingekuwa.

170 Lakini, mnaona, hawatapokea Karama yao. Tumetumiwa Karama kuu. Mungu alimtoa Mwanawe, wakaikataa. Ilikuwaje kwa Israeli? Wamekuwa katika machafuko tangu wakati huo. Mungu aliwatumia Mataifa, katika siku za mwisho, Roho Mtakatifu, nao wanamkataa. Ni kitu gani? Machafuko, hukumu.

171 Tokeni Sodoma, hata msiangalie nyuma. Msijifananishe na baadhi ya mambo haya hapa ya kisasa, tazameni Kalvari, endeleeni kuangalia huko. Msijali jinsi kanisa lilivyo kubwa, kama ni misheni moja pembeni, ni maskini maskani ndogo,

ama chochote kile, na hao wengine wanaokwenda kwenye maeneo haya makubwa sana, msiwajali; tazameni Kalvari. Naam, bwana. Kaeni na mtu wenu wa Mungu anayewafundisha Neno, na mdumu moja kwa moja naye, dumuni moja kwa moja na Kristo, na mwendelee kusonga mbele. Angalieni. Halafu . . .

172 Mnajua, njia pekee ambayo waliwahi kutuma ujumbe wakati huo ilikuwa ni mdomo kwa sikio. Sasa, wana simu, televisheni, chochote kile. Lakini wakati misafara ingepitia pale, ikienda pande za ulimwengu, kila mtu angetazama na kuona uwezo huu mkuu aliokuwa nao Sulemani. Na, mwajua, hatimaye ilishuka hadi Kusini; ilikuwa ni Malkia wa Sheba, ndiye huyo.

173 Na kama mkitaka kupima umbali wake, i—ilikuwa pande za mwisho za dunia iliyojulikana wakati huo. Yesu alisema pande za mwisho kabisa za—za dunia, hiyo ni kosmosi, ulimwengu, utaratibu wa ulimwengu, unaona, si dunia, ulimwengu, na hivyo basi, hizo zilikuwa pande zake za mwisho.

174 Naye maskini Malkia huyu alikuwa mpagani. Na kila wakati mtu alipoingia katika ufalme wake, kasema, "Loo, laiti ungaliiona Israeli! Mbona, wanaye Mungu huko juu, naye huyo Mungu anajiwakilisha Mwenyewe katika mmoja wa watu wao! Nao wote wako katika nia moja." Loo, jamani! Laiti sisi Wapentekoste tungeweza tu kuwa hivyo! Mnaona?

175 Loo, hakuna mtu angeweza kuzungumza dhidi ya Sulemani. "Loo, laiti ungalimsikia mchungaji wetu. Loo, nakwambia, ni jambo la ajabu sana. Laiti ungaliuhudhuria huo mkutano wakati mmoja. Loo, Mungu ametupatia karama kuu!" Kila mtu katika moyo mmoja na nia moja.

176 Ikiwa Wapentekoste, bila kuacha ulimwengu wote, laiti wangeninii tu, wote wangekusanyika tu pamoja na kuendelea na kuwa na madhehebu yao, bali wawe kitu kimoja! Tunacho Kitu ambacho ni halisi, sio, "*Huko*, kiota cha mwewe, wao hawanacho," na, "kiota cha kunguru *hapa*, hawanacho." Lakini hao ni ndugu zangu. "Njoni, tushauriane," chukueni tofauti zenu ndogondogo na kuzitatua, na kupata maelewano mazuri, kisha mwendelee, kama watu hawa walivyofanya kwa mkutano huu. Mnaona? Ikiwa inaweza kufanywa hapa, inaweza kufanywa kote. Ni Shetani akijaribu kulipiga vita na kuliondolea jambo hilo. Ni hayo tu. Kisha tunakusanyika na kweli tunaweza kukusanyika mahali fulani kwa ajili ya Mungu.

177 Sasa, kwa hiyo, mwajua, imani chanzo chake ni nini? Kusikia. Maskini Malkia huyo, kuna jambo fulani kwamba alikusudiwa Uzima; bila shaka, "Wote aliowajua tangu zamani aliwaita. Hakuna mtu angeweza kuja . . . Wote alionipa Baba watakuja."

178 Kwa hiyo hapana shaka ilikuwa kwamba, alikuwa amekusudiwa Uzima. Basi mara ya kwanza Neno hilo

lilipoangaza, Kitu fulani kilimgusa, “Ningependa kupanda huko juu. Ningependa kuliona.” Vema.

Msafara mwingine ukipitia, ukipitia huko, ninaweza kumwona akitoka, na, “M—Mtukufu, Malkia!”

“Naam. Mlipitia njia gani?”

“Tumetoka kaskazini.”

“Je, mlipitia Palestina?”

“Naam.”

179 “Naweza kukuona kwenye kasri peke yako? Aisee, je, ni kweli kuhusu Israeli kule juu, kwamba Mungu wa kimbinguni, Mungu wao, Mungu wao mmoja, anajiwakilisha Mwenyewe katika mmoja wa watu wao?”

“Ni kweli, na—nakwambia. Nilisikia habari zake nilipowapitisha ngamia wangu, ni—nilivumilia kwa siku chache na kutazama, na ni kweli.”

“Loo, asante, Bwana! Asante. Unaweza kuondoka.” Katoka nje.

180 Moyo wake ukaanza kuwaka. Kuna kitu kuhusu unaposikia habari za Mungu! Mwanadamu sikuzote ananinii . . . Anajua alitoka mahali fulani gizani, naye anajua kwamba hana budi kurudi kwa njia hiyo pia. Anajua alikuja ulimwenguni kwa njia ya kisiri, anatoka vivyo hivyo. Yeye daima anajaribu kuangalia kupita pazia.

181 Angalieni. Ndipo, loo, jamani, siku moja aliamua atajionea mwenyewe. Hiyo ndiyo njia. Usikae nyumbani, ukikosoa, nenda upate kujua. Kwa hiyo ana—anajiandaa. Sasa, mnakumbuka, maskini msichana huyo alikuwa na matatizo. Sasa, nilikuwa nikiwakemea ninyi akina dada, sasa nitawaambia kuhusu mwanamke halisi, mnaona. Angalieni, mwanamke huyu mdogo alikuwa na ugumu fulani. Sasa, jambo la kwanza, akiwa mpagani, ilimbidi aende kumwona baba mtakatifu wa kanisa lake, mnaona, ambapo angepata ruhusa; yeye ni Malkia, kumbukeni.

182 Kwa hivyo ninaweza kumwona akishuka kwenda kwa kuhani mtakatifu, ndipo akasema, “Ee, Kasisi Baba Mtakatifu sana, nimesikia ya kwamba, kule Israeli, wana uamsho kule juu, na ishara na maajabu yanatukia ya Mungu wa kimbinguni ambaye amempaka mtu mafuta kwa Roho Wake, naye ananena kama Mungu.”

183 Ninaweza kumwona baba mtakatifu akisema, “Sasa, angalia, mtoto wangu, wewe ni Malkia, una fahari, wewe ni mfuasi wa kanisa hili kubwa, hutaki kamwe . . . hutaki kuwa na ninii yoyote . . . Huyo ni mtakatifu anayejibingirisha,” ama, loo, vema, unajua. “Ni . . . Hutaki kuingia katika kundi la aina hiyo. Hawana chochote. Wana . . . Unasikia upuuzi huo

kila wakati. Sikuzote tumesikia kuhusu ‘kufungua Bahari ya Shamu’ na kadhalika. Ni bure. Kama jambo lolote lingeendelea, lingeendelea katika madhehebu yetu hapa, lingekuwa papa hapa tunapolipata, hapa ndipo linapopaswa kuwa. Je, unamwona yule Dagoni mkuu, mtakatifu pale?”

184 “Naam, nilimwona. Nimekuwa nikimtazama, nyanya yangu alimtazama, nyanya wa nyanya yangu alimtazama, na nyanya wa nyanya wa nyanya yangu alimtazama, hajawahi kusogea. Wananiambia kwamba Mungu huyu anajifanya Mwenyewe halisi ndani ya mwanadamu.”

185 Mnajua nini—mnajua uabudu sanamu ni nini? Mwabuduo anasujudia mbele ya sanamu, na kwa mungu wa kufikirika kwa akili ya kufikirika, anawazia huyo mungu anamjibu. Ni kinyume jinsi gani na Ukristo! Yeye anamchukua mtu aliye hai, na kujimimina Mwenyewe ndani ya huyo mtu, na kumfanya sanamu. Amina. Haleluya! Hivyo ndivyo alivyofanya kwenye siku ya Pentekoste.

186 Mnafikiri nina wazimu nikipiga kelele, “Haleluya”? Inamaanisha, “Mungu wetu asifiwe.” Kwa hivyo, lakini angalieni. Sijasisimkwa sasa, ninajua mahali nilipo hasa, mnaona, ninajisikia vizuri tu.

187 Angalieni. Ndipo tunapopata . . . Na hii . . . Yeye alisema, “Sasa, angalia, ewe Binti, ukianza kujipumbaza huku, ulokole kama huo, itanibidi tu kukupa karatasi yako ya kanisa.”

188 Ninaweza kumwazia, akisimama pale kidogo, na kusema, “Vema . . .” Unajua, ikiwa Mungu amenena na moyo wako, hakuna kitakachokuzuia, maana imani huja kwa kusikia. Wewe shika imani, wala hakuna kitakachokuzuia, hivyo tu, utaenda kwa vyovyote vile. Kwa hiyo imani chanzo chake ni kusikia, ndipo akasikia, naye, moyo wake ulikuwa ukiwaka ndani yake kuiona, alitaka kuona kama ni kweli au la.

Ninaweza kumwazia akisema, kasema, “Afadhali unipe tu makaratasi yangu.”

189 “Wewe ni Malkia! Utapoteza heshima yako. Unaishi katika ujirani bora kuliko watu wa aina hiyo.” “Unaendesha gari bora zaidi, wajua,” na upuuzi wote wa namna hii, unajua. Na kwa hiyo, sasa alikuwa na mengi ya kumkabili.

190 Kwa hivyo anaenda nyumbani, naye anawazia, “Sasa, sijui. Nimesoma baadhi ya Magombo ambayo baadhi ya hao watu wamenipa, na inaonekana kana kwamba ikiwa huyo alikuwa ni Mungu, kama huyo ni Mungu, basi kama anajiwakilisha Mwenyewe, jinsi anavyoandika Maneno Yake *Hapa*, ndani ya mtu huyo, vema basi, hakika huyo hapana shaka ni Mungu.”

191 Na sasa, nawaambia alichofanya. Alitoka na kuchukua vito vingi, dhahabu nyingi, na ubani mwingi, na zawadi nyingi za thamani kuu, naye akasema hivi: “Nitaenda nazo, na ikiwa ni

kweli, nitaiunga mkono; kama si kweli, ninaweza kurejesha pesa zangu moja kwa moja."

192 Angeweza kufundisha wengi wetu sisi Wapentekoste hekima fulani. Kuachilia kanisa lenu wenyewe lifilisike huku mkiunga mkono kitu fulani kwenye redio, ambacho kitawacheka, kiwadhihaki, kitu kile kile mnachoamini. Na bado, mnaenda . . . Hakuna haja ya kuwa mwangalifu juu ya hilo, mnajua ni kweli. Saidieni kanisa lenu wenyewe. Baadhi ya upuuzi huu hapa nje huwadhihaki, na kuwaita watakatifu wanaojibingirisha, wanakana imani yenyewe, na—na upuuzi kama huo, na bado, mnauchangia! Nisingekuwa na hivyo vitu nyumbani mwangu. Hiyo ni kweli.

193 Mimi ni Mpentekoste, nami ninaamini katika Roho Mtakatifu kutoka utosi wa kichwa changu hadi chini ya miguu yangu, na kote ndani yangu, moyo, nafsi, na mwili. Ninamwamini Mungu, ninaamini Neno, ninaamini ni Kweli, wala sitaki kuunga mkono kitu hicho. Kwa hiyo angeweza kutufundisha jambo fulani.

194 Sasa, akapakia ngamia wake. Sasa, kamwe hakuwazia . . . Kumbukeni, pamoja na hazina hiyo yote, akipitia kwenye jangwa hilo! Pia sikilizeni, si safari fupi. Mnajua ilichukua muda gani juu ya ngamia? Siku tisini. Sasa, yeye hakuwa na Kadilaka yenye kiyoyozi kuninii . . .Ilimbidi kuvuka Sahara, hivyo ilimchukua siku tisini juu ya ngamia.

195 Si ajabu atakihukumu kizazi hiki, wengine hawatavuka barabara, hawatapiga kona kwenye Kadilaka yenye kiyoyozi. Hiyo ni kweli. Mnaona? La, hawatafanya hivyo, lakini alichukua safari ya siku tisini, isitoshe, wana wa Ishmaeli walikuwako jangwani siku hizo, wanyang'anyi, huku ana hazina hiyo yote.

196 Lakini *kwa njia moja au nyingine*, unapodhamiria kumwona Yesu, hakuna kitu kitakachokuzuia, utaenda kwa vyovyote vile; huoni hatari. Kasema, "Mumeo ataitoroka nyumba yenu." "Mke wako hatakupokea tena." "Baba, mama watakufukuza." "Watakutupa nje ya kanisa." Huoni mambo hayo, unajaribu kumfikia, unajitahidi tu uwezavyo kufika Huko, maana kitu fulani moyoni mwako, kinawaka.

197 Sasa, akaanza kuvuka jangwa, ndipo alipofanya hivyo, labda ilimbidi kusafiri usiku. Alikuwa na vijakazi wake wachache na matowashi wake. Vema, hizo zingekuwa nyara rahisi jinsi gani kwa watoto wa Ishmaeli! Kuliua tu kundi hilo la matowashi na kuchukua dhahabu hiyo yote na kadhalika, iliyokuwa imewalemea hao ngamia, ingekuwa rahisi. Lakini, mnaona, Mungu daima hukutengenezea njia kama unataka kumfikia. Sijui jinsi anavyolifanya, lakini atalifanya. Wakati hakuna njia, basi Yeye ndiye Njia. Anapatengenezea njia.

198 Sasa, huyo akavuka hilo jangwa. Akawasili. Sasa, yeye hakuja kama watu wengi, jinsi mnavyowaona, nimewaona papa

hapa mkutanoni, unasimama, unachukua somo, kisha unasema maneno mawili matatu hivi ambayo watu wanasema, "Naam, sijui kuhusu hilo. Kamwe siwezi kuelewa hilo." Mnajua nini? Wataamka na kutoka nje, hawatakusikiliza. Kisha unachukua tena, wanaonekana tu kana kwamba hawataki ku—kulizingatia Hilo. Na kama—na kama ukikaa kwa muda mrefu kidogo, labda, tuseme umechelewa kwa nusu saa ama *kitu kingine* namna hiyo, loo, jamani! Hmm! Kamwe hawawezi kustahimili.

199 Wakati Paulo alipohubiri Injili iyo hiyo usiku kucha, mvulana mmoja alianguka kutoka dirishani na akafa. Walifikiri ingewalazimu kutuletea mmoja jana usiku, mtoto mchanga, lakini Bwana alimsaidia.

200 Lakini angalieni, angalieni kilichotukia. Basi akaja, akachukua vya kutosha . . . Akafungua mizigo ya ngamia zake na kadhalika huko nje katika uwanja wa ikulu, naye alikuja kukaa, na kusoma Magombo mpaka ashawishike kabisa.

201 Loo, ni mwanamke mzuri jinsi gani! Ninamthamini maskini mama huyo, alikuwa anaenda kukaa mpaka aliposhawishika. Alikuwa akisoma Magombo yote ya nabii Isaya, na vingine vyote mbalimbali, na hao wengine waliokuwa wameandika, na Vitabu vyote vya Musa, na jinsi walivyovuka Bahari ya Shamu, alitaka kuona Mungu huyo alikuwa ni nani.

202 Kwa hiyo akaja, naye akawachukua wajakazi wake na kadhalika, akapiga hema yake, ndipo kesho yake asubuhi, akaingia kanisani. Nami nawazia kulikuwa na umati mkubwa pale asubuhi hiyo, nao walikuwa wakicheza muziki wote wa Mungu, na baragumu zikilia, na kadhalika, na, jamani, hao wote, jambo la kwanza, wote wakanyamaza, ndipo baada ya kitambo kidogo, Mchungaji Sulemani akajitokeza, akapanda jukwaani, mtu aliyeonekana wa kawaida.

203 Sijui alizungumzia nini asubuhi hiyo, lakini chochote kile, kilimgusa maskini huyo Malkia, akaanza kuona hiyo hekima. Huenda alingoja hadi akapata kadi ya maombi, kwa hivyo hata hivyo a—alisubiri hapo. Baada ya kitambo kidogo, ukafika wakati wake wa kuja mbele zake, nayo Biblia ilisema alipokuja mbele ya Sulemani, hakukuwa na jambo lolote alililofichwa Sulemani, alimwambia siri zake zote. Haleluya!

204 Hiyo ilikuwa ni karama ya upambanuzi. "Na, tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa." Naam. Akamwambia . . . Biblia ilisema hapakuwa na jambo lolote alilofichwa Sulemani, alisimama pale tu, na kumchukua, labda huyo mmoja tu, na kulifunua tu, na kumwambia yale aliyokuwa amefanya, na vile mambo yote yalivyokuwa, akayafunua.

205 Hivi hamwoni? Ni Mungu yeye yule. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na hapo uliposimama Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, na kuitwa ibilisi. Si ajabu alikuwa akiwakemea.

206 Mwangalie huyo maskini Malkia sasa. Ninafunga. Mara ya kwanza alipopata kuona kitu chochote kilicho halisi. Akaligeukia kusanyiko, kwanza, akawageukia watu waliokuwa pamoja naye, naye akasema, "Heri ninyi mlio pamoja na karama hii wakati wote. Heri ninyi mnaoweza kuona haya kila siku, heri macho yenu." Wazieni mpagani! "Macho yenu yana heri, ninyi mnaoweza kusimama na kuyaona haya," ninyi Wapentekoste, "heri macho yenu, kwamba mnaliona kila wakati."

207 Hata alitaka kuchukua udongo arudi nao nchini mwake. Ati nini? Alikuwa ameona kitu halisi kwa mara yake ya kwanza. Alikuwa ameona sanamu nyingi sana, na theolojia, na uigaji mwingi sana, lakini pasipo na mwenendo halisi wa Mungu, naye alipomwona Mungu kweli akitenda kazi, alilishika. "Naye Malkia wa Kusini atasimama siku ya Hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa, kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa." Maskini huyo jamaa aliiona tu kwa mara yake ya kwanza.

208 Katika kufunga, naweza kutoa tamshi hili dogo, huenda niliwaambia kulihusu hapo awali. Mimi huwinda, hiyo ni burudani yangu, kupiga shabaha, kuwinda, kuvua samaki. Mama yangu mkongwe, ambaye ndiyo kwanza aage dunia, alikuwa chotara, kwa hiyo, wala wongofu wangu haukuiondoa kamwe, bado napenda mambo ya porini, namwona Mungu.

209 Nilizoea kuwinda kwenye misitu ya kaskazini. Kuna jamaa huko aitwaye Bert Call, mmoja wa wawindaji bora sana niliowahi kuwinda nao. Haikukubidi kuhofu utampoteza, alijua jinsi ya kurudi nyumbani. Naye alikuwa mwindaji mzuri, lakini alikuwa mtu katili kuliko wote niliyepata kumwona. Sijawahi kumwona mtu, alikuwa na macho kama mjusi, wala si—sijawahi kuona m—mtu katili zaidi maishani mwangu. Loo, alikuwa katili kweli. Naye alikuwa akipiga risasi watoto wa kulungu tu, mnajua watoto wa kulungu ni nini, kulungu wadogo, alikuwa anawapiga risasi ili tu nijisikie vibaya. Sikuzote nimechukia kuwauwa jamaa wadogo. Na—naye—naye angewapiga risasi tu. . .

210 Sasa—sasa, kama sheria inasema unaweza kumpiga risasi mtoto wa kulungu, kumbuka, hiyo ni sawa, nilikuwa mlinzi wa wanyamapori kwa miaka mingi, na kwa hiyo, ikiwa sheria inasema unaweza kuwapiga risasi watoto wa kulungu, ni sawa. Sio u—ukubwa, jinsia, ama mnyama yeyote yule, ni kama wanakuruhusu kumpiga risasi au la. Ibrahimu alimchinja ndama na kumlisha Mungu, kwa hiyo si lolote kuhusu sehemu yake *ndogo*.

211 Lakini kuwa katili tu, hayo ni mauaji kwangu mimi, hiyo ni kweli; kuua kwa kujifurahisha tu, hilo si sawa. Hupaswi kamwe kuchukua zaidi ya kile ambacho sheria

inasema, na ukichukue kwa heshima na ubinadamu. Kila kitu unachofanya, kifanye vizuri, hiyo ni kweli, kwa sababu nyinyi ni "nyaraka zilizoandikwa zinazosomwa na watu wote," jinsi unavyojiendesha, na mambo mnayofanya kama Wakristo.

212 Lakini Bert angefanya hivi kwa ukatili tu, alikuwa jamaa katili. Kila wakati ningepanda huko a—amwone mtoto wa kulungu, angemlipua tu, ili tu kunifanya . . . labda hata asimwokote, ili tu kuwa katili.

213 Mwaka mmoja, nilienda huko kidogo nimechelewa, nilitoka kazini nimechelewa, nasi tulikuwa na msimu mbaya. Nao msimu wa kuwinda ulikuwa umemaliza majuma mawili au matatu, na hiyo ilikuwa huko New Hampshire, ilikuwa—ilikuwa huko tu kwenye Safu ya Rais, nayo ilikuwa ni—ilikuwa nchi nzuri sana ya kuwindia kulungu mwenye mkia mweupe. Nafikiri mna nyumbu hapa, naye ni mwenda pole na goigoi ukimlinganisha na hao.

214 Nena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kutoroka, unapaswa kuona mkia mweupe wakati ameshikwa na woga, anaweza tu kutoweka. Kwa hivyo huna budi kuwa mwindaji na mwenye shabaha. Usimlemaze, mwue, na, ikiwa utamwua, usipomwua, achana naye. Kwa hivyo inahitaji mwindaji mzuri mwerevu kupata kulungu wake. Kwa hivyo napenda kufanya hivyo.

Kwa hiyo basi, wakati tungeenda kuwinda . . . Tulienda kuwinda, akasema, "Billy, umechelewa kwa takriban majuma mawili." Kasema, "Tuna takriban juma moja tu."

Nikasema, "Naam, lakini Bert, hakika tunaweza kumpata mmoja mahali fulani."

"Kumekuwa na upigaji mwingi risasi."

215 Ndipo ikaja theluji usiku huo, kama inchi sita ama nane, kama mahali pazuri pa kufuatilia. Na kila wakati tulibeba themosi iliyojaa chokoleti moto, ambapo, kama tungegeuka msituni na kulazimika kukesha usiku kucha, mbona, lisingetusumbua, mnaona, na kuwasha moto.

Hivyo basi, Bert akasema, "Nina kitu fulani kwa ajili yako, Billy."

Nikasema, "Ni nini?"

Kasema, "Nitakuonyesha." Akanyoosha mkono na kutoa filimbi ndogo, akaipiga, nayo ikasikika kama mtoto wa kulungu anayemwita mama yake, mwajua, ma—maskini mtoto wa kulungu, mnajua jinsi wanavyopiga maskini kelele hizo za ajabuajabu.

Nikasema, "Bert, u—usingefanya hivyo."

Akasema, "Aw, hivyo ndivyo ilivyo kwenu wahubiri, nyinyi ni waoga sana." Kasema, "Hutawahi kuwa mwindaji," kasema, "wewe ni mwoga sana."

Nikasema, “Bert, kuna kitu kama kuwa mwoga kupindukia, na kitu kama kuwa wazimu.” Mnaona? Nami nikasema, “Wewe—wewe—wewe ni wazimu kufanya kitu kama hicho. Usifanye hivyo,” Nikasema, “huo ni ukatili.”

Akasema, “Aw, jirudie, Mhubiri. Hima, haya twende.”

216 Basi nikachukua bunduki yangu, tukasafiri, loo, karibu hadi saa sita mchana, hatukuona mburuzo wowote. Basi ulikuwa ni usiku wa mbalamwezi pia, mwajua, nao watakula wakati wa usiku, kisha waingie kichakani na chochote kile. Watajificha saa za mchana, na karibu watajiua kwa njaa, kwa kuwa wamerushiwa risasi. Na kwa hiyo, hata hatukuona mburuzo, ilikuwa karibu adhuhuri.

217 Na kwa hiyo, Bert akaketi chini, chungu dogo la theluji ambapo pepo zilikuwa zimeipeperushia karibu na vichaka, kulikuwa na uwazi karibu mara mbili ukubwa wa jengo hili. Na kwa hiyo Bert akaketi pale, naye a—akaingiza mkono ndani, namna *hii*, nilidhani alitaka kuchukua themosi yake na kunywa ile chokoleti moto. Tungekula sambusa zetu kisha tutengane, angeelekea upande mmoja kupitia Ujia wa Jefferson, ama kwa njia fulani, nami ningerudi kupitia Washington, kwa kawaida njia fulani huko, nasi tungeweza kukutana saa tatu au nne kwenye kambi kituoni. Kama tungempata kulungu yeyote, tungemtundika juu, kesho yake, tumchukue farasi ama chochote kile, tumwendee.

218 Hivyo basi, nilifikiri alikuwa anajiandaa tutengane pale pale, maana tulikuwa tukipanda juu sana; hakuna, hakuna mengi kupita misitu kule. Kwa hiyo akaketi, akanyosha mkono nyuma namna *hii*, naye akatoa hiyo filimbi ndogo. Nami nikasema, “Loo, Bert, usifanye hivyo.” Kaona hayo macho ya mjusi yakinitazama, na kutabasamu tu kama ninii, sijui nini. Akaiweka maskini filimbi hiyo kinywani na kuipiga, nayo ikasikika tu kama mtoto wa kulungu, mwajua, jinsi anavyomlilia mama yake. Naye alipofanya hivyo, ng’ambo tu ya ule uwazi, kulungu jike mkubwa mno akasimama, kulungu jike ni mama kulungu, mnaona, akasimama. Ningeweza kuona hayo macho makubwa ya hudhurungi yakitazama huku na huku, hayo masikio makubwa yaliyochongoka.

219 Ilikuwa ni nini? Alikuwa mama, mtoto alikuwa ameita, alikuwa taabuni. Akasimama, iwe mchana ama si mchana, hatari ama hakuna hatari, alikuwa mama; alizaliwa mama. Kuna kitu ndani yake, kama, hata msichana mdogo anayecheza na mwanasesere, ni nini hicho? Amezaliwa kuwa mama. Mnaona? Kiko ndani yake, ni kwa kuzaliwa. Hakuwa mnafiki, hakuwa akiigiza kitu, alikuwa mama.

Ndipo Bert akanitazama namna *hiyo*, na hayo macho ya mjusi yakanitazama tena.

Nikasema, “Usifanye hivyo, Bert. Usifanye hivyo, Bert.”

220 Akainama namna *hiyo*, naye akaipiga kwa urahisi sana, mama kulungu huyo akatoka moja kwa moja kwenye ule uwazi. Sasa, hilo si la kawaida, sana. Wakati huo wa mchana, na kulungu mkia mweupe, hakika kulikuwa kurushwa kwingi kwa risasi kulikoendelea, hawatafanya hivyo. Sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Akatoka hapo nje, nje kabisa, uwazi. Nikamwona . . . Hatubebi risasi kwenye mtutu hadi uwe tayari kupiga risasi. Kwa hiyo nikamwona akitoa hii .06 na kuweka hiyo risasi kubwa ya uyoga uzito wa mia na themanini kule juu. Alikuwa mwenye shabaha hodari sana. Nikamwona akilenga namna *hiyo*, nayo hayo macho ya mjusi yakiangalia kwenye darubini hiyo, nyuzi hizo za shabaha zilikuja moja kwa moja kwenye moyo wake.

221 Wakati—wakati bolti iliposhuka, huyo kulungu alisikia hiyo bolti, naye akageuka, hayo masikio makubwa yaliyochongoka namna *hiyo*. Nami nilikuwa nimesimama nyuma ya kichaka fulani. Naye akatazama pale pale, vema, akamwona huyo mwindaji, lakini yeye alikuwa mama, mtoto wake mchanga alikuwa taabani, kifo au si kifo, alitaka kumchukua mtoto wake. Naye . . .

222 Niliona hiyo bunduki imelenga vilivyo, hizo neva tulivu za jamaa huyo, nikawaza, "Loo, Bert, unawezaje kufanya hivyo? Dakika moja kutoka sasa utaulipua huo moyo wa mama mwaminifu mpaka upande wake wa pili." Mnaona? Karibu sana naye, hakuwa zaidi ya yadi thelathini. Nikawazia, "Loo, jamani! Ata—ataulipulia mbali moyo wake kwenye umbali huo, risasi hiyo kubwa namna *hiyo* na hiyo . . ." Nikawazia, "Unawezaje kumwua mama huyo anayemtafuta mtoto wake, na kucheza sehemu ya mnafiki kumtoa hapa hadharani namna hiyo? Naye huyo hapo akionyesha kuwa yeye ni mama halisi. Afe asife, mtoto wake yuko taabuni!"

223 Nisingeweza kuliangalia, nikageuza kichwa changu *hivi*, nikasema, "Baba wa Mbinguni, usimruhusu kufanya hivyo. Usimwache afanye hivyo, Bwana. Loo, anawezaje kufanya hivyo? Anawezaje kuwa katili kiasi cha kumwua kulungu huyo hivyo? Anawezaje kufanya hivyo? Na maskini mama huyo pale, akionyesha uaminifu huo na upendo kwa ajili ya mtoto wake mchanga, halafu atamwua hivyo. Mbona? Usimwache afanye hivyo, Bwana." Nilikuwa tu nikiomba moyoni mwangu. Nami, nikingojea kusikia bunduki hiyo ikifyatuka wakati wowote, basi nikawaza, "Mara tu ikifyatuka, yote yamekwisha."

224 Nilikuwa nimesimama futi mbili au tatu kutoka kwake. Alikuwa amepiga magoti karibu na chungu cha theluji, chungu cha namna *hii*, na papo hapo juu ya kichaka fulani; kulikuwa na uwazi papo hapo. Nami . . .

225 Sasa, mara ya mwisho nilipomwona, alikuwa ameishikilia hiyo bunduki namna *hiyo*. Loo, jamani! Unyamavu, sikusikia

mlio wa bunduki, nikawaza, "Kwani kuna nini?" Nilikuwa nimegeuza mgongo wangu *hivi*, nilikuwa . . . Nisingeweza kuitazama. Nikageuka na kuangalia, nao mtutu wa bunduki ulikuwa ukienda *hivi*, ukitikisika. Akaangalia pande zote, machozi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake, akaichukua hiyo bunduki na kuitupa kwenye hicho chungu cha theluji, akanishika mguu wa suruali *hivyo*, na kusema, "Billy, nimetosheka. Niongoze kwa huyo Yesu unayezungumza habari zake."

226 Pale kwenye chungu hicho cha theluji, nilipiga magoti kando yake, na kumshika mkono. Yeye ni shemasi kanisani sasa. Ilikuwa ni nini? Aliona kitu halisi, kitu ambacho hakikuwa cha kujifanya, upendo halisi wa mama ukimwita mtoto wake. Aliona kitu ambacho hakikuwa cha kuigiza, wala unafiki, kitu ambacho kilizaliwa ndani yake.

227 Ndugu, dada, hicho ndicho ulimwengu unachoonea njaa siku hizi, wenye mioyo iliyo na njaa, ni kuona kitu halisi, Mungu halisi, sio udanganyifu fulani unaofanywa kupitia theolojia fulani ya kiakili, bali Mungu halisi, wa kweli, na watu halisi, wa kweli kumwakilisha Yeye. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, "Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, na kuwahukumu kuwa wamekosa, kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa."

228 Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi. Kabla hatujaitisha mstari wa maombi, ninataka kuuliza swali. Iweni wakweli kwangu moja . . . Tunafunga sasa, labda, wengine kwa mara yetu ya mwisho kuonana, baadhi yenu.

229 Sa—sala ndogo tu kimyakimya moyoni mwako. Ni wangapi hapa ndani wangependa kuwa Mkristo kadiri kulungu huyo alivyokuwa mama? Si ungetaka? Hiyo ni kweli. Roshani? Ungetaka kuwa Mkristo kadiri kulungu huyo alivyokuwa mama, hata unaweza kuonyesha upendo wako kwa Mungu kwa uaminifu kama kulungu huyo? Kwa nini? Alizaliwa mama, alikuwa mama. Je, unataka kuwa Mkristo wa kweli hivyo? "Nife nisife, hata iweje, nataka kuwa Mkristo, halisi." Mtu mmoja kwenye roshani? Mikono miwili au mitatu tu, ambapo kuna mia moja kwenye orofa ya chini. Mungu awabariki. Hilo ni jema. Na—najua Mungu yuko huko juu, vivyo hivyo. Unafikiri uko mbali sana na Mungu? La, Yeye yuko kila mahali.

Na tuombe sasa. Je, kila mkono ulioinuliwa . . . ? Kumbukeni, Yeye aliuona mkono wako, huwezi kujongea bila Yeye kuuona.

230 Baba yetu wa Mbinguni, tunakaribia mwisho sasa. Dakika chache, mstari wa maombi utakuwa unaanza, hao watu, wanakuja kuombewa, nasi tunafikiri hivyo "Tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa." Tumekuwa na yapata miaka elfu

mbili mia tano ya kuandika Maandiko ya Mungu. Ni Maandiko mangapi zaidi . . . Jinsi ilivyo kuu zaidi leo, kwenye Uzima wa Yesu Kristo! Jinsi alivyosema ya kwamba angekipa kizazi kiovu na cha zinaa ishara ya ufufuo!

231 Ee, Baba, tunaona kitu Fulani halisi, tunamwona Yesu. Tunamwona katika Kanisa Lake, tunamwona akizungukazunguka, akifanya kazi alizofanya alipokuwa hapa duniani. Inaigusa mioyo yetu, Bwana. Tufinyange, tunashuka kwenye nyumba ya Mfinyanzi sasa, tuvunje, Bwana, na kutufinyanga, na kutufanya Wakristo halisi. Utupe kuzaliwa upya, ninii . . . tupe Roho wa Mungu ndani yetu kama roho ya umama ilivyokuwa ndani ya kulungu huyo. Tujalie, Bwana.

232 Kila mtu aliyeinua mikono yao, tunawaombea, Baba, ya kwamba utawatimizia haja yao. Kama sitawahi kuwapa mkono humu duniani, naomba nifanye hivyo katika Nchi iliyo bora zaidi. Tujalie, Bwana.

233 Kwa sababu ya onyesho hilo, nadhani, labda huyo mama kulungu angali hai hata wa leo. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba utawapa maisha marefu na huduma kuu kwa ajili Yako. Wasamehe dhambi zao. Huenda kulikuwa na wengine hapa ambao hawakuinua mikono yao, washughulikie, Bwana, wajalie kujua walichokosa kwa kutokumjua Mwanao, Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Yuko hapa leo, naomba, Baba, kwamba utamfanya adhihirike sana, hata watu wataona ya kwamba Yu hai bado, aliye mkuu kuliko Sulemani. Tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

Tutaimba tu wimbo huo, pamoja, kabla hatujaanzisha mstari wa maombi.

Natumaini tu ustahilifu Wako,
Je, ningeutafuta uso Wako; (Je, ungependa kuuona uso Wake? Tazama.)
Iponye roho yangu iliyojeruhiwa, na kuvunjika,
Loo, niokoe kwa neema Yako.

Mwokozi, (Loo, mlete tu papa hapa. Loo, tutawaleta huko chini.)
. . . kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Loo, usinipite.

Sasa, kwa kuinamisha tena vichwa vyetu, kidogo, huku mikono yetu imeinuliwa, uimbeni kwa upole sana pamoja nami sasa.

Mwokozi . . .

Wewe ambaye ni mhitaji, achilia kila kitu.

Sikia . . . kilio kinyenyekevu;
Wakati wengine Wewe . . .

Ponya, leso hizi, Bwana, watu ambao zinawaendea katika Jina la Yesu.

Usinipite.

234 Anayeishi milele, aliyepo daima, tayari kusaidia, kuponya . . . Sasa, ninaamini kuna takriban kadi mia mbili za maombi zilizosambazwa. Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Mkutano unafunga sasa, nanyi watu mnaomkubali Kristo, fanyeni hivi, fanyeni hivi, jambo halisi. Naamini mlimaanisha. Mwendeeni mmoja wa wachungaji hawa, mwaambie mnataka kubatizwa, kisha mkae huko, watawaelekezeni jinsi ya kuwachukua, tangu hapo na kuendelea. Fanyeni hivyo, sivyo?

235 Msiache tu lishuke wakati uamsho umepita, endelea, uwe Mkristo halisi, aliyezaliwa, acha Roho wa Mungu aingie ndani yako. Utakuwa Mkristo kama vile huyo mama kulungu alivyokuwa kulungu, mama. Sasa, fanyeni hivyo, sivyo? Nitawaamini, nitaamini nitawaona tena Ng'ambo ya pili, nisipowaona huku tena.

236 Sasa, tunatambua ya kwamba, kumchukua mmoja mmoja chini ya upambanuzi huo alasiri ya leo, ningepata takriban nusu dazeni, nami ningeanguka. Tunajua hilo. Ni wangapi wanaelewa hilo? Hakika. Mnaona, usingeweza kufanya hivyo. Lakini mnaamini, baada ya siku hizi zote usiku kupita, kila usiku, je, mnaamini ya kwamba ni Mungu? Basi mimi . . . Asanteni.

237 Sasa, ili Uwepo Wake utakuwa pamoja nami, nitamwomba sasa, ya kwamba, kama atafanya, hapa mkutanoni, yale aliyofanya alipokuwa duniani. Sasa, kama nikitazama chini na kuona, labda, msichana huyu aliyeketi *hapa*, nami ningesema, "Yeye ni kiwete," mtu yeyote anaweza kuona hilo. Mnaona? Lakini vipi kuhusu mtu fulani huko nje ambaye anaonekana kuwa na afya na nguvu?

238 Sasa, hebu niseme jambo hili mara nyingine tena. Kama Yesu Kristo, Bwana wetu, angekuwa amesimama hapa leo, kama vile ninavyosimama, amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kukuponya. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Tayari ameshafanya hivyo, "*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*."

239 Sasa, alipokufa, alifanya upatanisho kwa ajili ya uponyaji, sote tunajua hilo. Ikiwa upatanisho wa kale ulikuwa na uponyaji, *huu* ulikuwa bora zaidi. Alisema, "Katika upatanisho wa kale," (Ni bora zaidi kiasi gani?), alisema, "'Usiue,'" ilimbidi kuua, kitendo, "Lakini, 'Yeyote anayemkasirikia ndugu yake bila ya sababu, ameua tayari.'" Agano la kale lilisema, 'Usizini.' Hili lilisema, 'Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.'" Mnaona? Ni kuu zaidi.

Kwa hivyo uponyaji uliinuliwa pia kutoka kwa ule wa kale hadi mpya.

240 Sasa, angalieni kwa makini sasa. Basi angefanya nini kama angalikuwa amesimama hapa? Jambo pekee angaliweza kufanya, lingekuwa ni kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Yesu. Je, hiyo ni kweli? Sasa, vipi kama mtu fulani atakuja hapa akiwa na makovu mikononi mwake, na—na—na makovu ya misumari *hapa*, chochote kile, miiba, na . . . ? Huyo angeweza kuwa mnafiki yeyote. Hiyo ni kweli.

241 Lakini jinsi unavyojua, Yeye alisema, "Kwa matunda yao mtawatambua." Watu hunena kwa lugha, wanadai kuwa wana Roho Mtakatifu, kisha wanatoka na kusema uongo na kuiba na kudanganya, hawana Roho Mtakatifu. Nimewaona wachawi wakinena kwa lugha, wakiweka penseli chini, inakimbia huku na huku kwenye bomba la moshi la stovu, na kucheza ule *Kunyoa Ndevu Na Nywele, Maradufu*, inashuka na kuandika kwa lugha isiyojulikana, naye mchawi anasimama pale na kuifasiri, na kuwaambia walichosema. Sasa, wewe . . . Umewaona wakinywa ninii ya binadamu . . . wakinywa damu kwa fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita ibilisi mpaka hizo nguvu zingekuangusha chini, na kunena kwa lugha. La, la, anaweza kuiga chochote, lakini maisha ndiyo muhimu.

242 Sasa, chukua uhai ulio katika mbalungi, ama, katika mpichi, kisha uuweke kwenye mtofaa, ungekuwa na tunda la aina gani? Kama uhai wa mpichi ulikuwa ndani ya mtofaa, ungekuwa na mapichi. Hakika. Kwa tunda! Sasa, wewe weka Uhai Wake *hapa*, ndipo utazaa kile alichokuwa. Tulionaje, juma hili, ya kwamba walijua Yeye alikuwa ndiye Masihi? Kwa sababu kwamba Yeye alikuwa Nabii ambaye Musa alinena habari zake, aliwaonyesha kwa ishara Zake. Na jinsi tulivyoipitia! Sasa, Yeye angali ni Kristo yeye yule leo. Mnaamini hilo?

243 Sasa, angalieni. Sasa, kumbukeni, Yeye aliahidi ya kwamba Mataifa wangepokea jambo lile lile, upambanuzi ule ule ambao Mungu alifanya katika mwili wa mwanadamu wa nyama kabla ya Sodoma kuteketezwa. Je, hiyo ni kweli? Sote tunaelewa hilo sasa? Mnaona, angalieni, kama ni vigumu kuelewa, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuja . . . " Kuna matabaka matatu ya watu: Wasodoma; na Lutu, kanisa vuguvugu, la kawaida, kanisa la kimadhehebu; na Ibrahimu, mteule, nje ya Sodoma; Kanisa lililoitwa litoke, na kanisa katika Sodoma.

Sasa, angalieni, sio wakati ambao utaangamizwa kwa maji, Alisema itakuwa, lakini kuangamizwa kwa moto, ambao sasa unapaswa kuangamizwa.

244 Angalieni, walikuwa na mhubiri, wawili wao kushuka kule chini, wajumbe wawili, na kuhubiri Sodoma. Naye Ibrahimu, Mjumbe wa . . . *huku* juu, Yule aliyebaki nyuma alifanya mwujiza

mbele ya Ibrahimu kwa kuelekeza mgongo Wake kwenye hema na kumwuliza Ibrahimu, akimwambia alichokuwa, na kuuliza . . . kumwambia Sara mkewe . . . Si S-a-r-a-i, bali S-a-r-a, ambapo, kabla tu ya hapo, alikuwa amebadilisha jina lao, kutoka lake, Abramu, likawa Ibrahimu; akamwita Ibrahimu, na mkewe Sara, akasema, "Yuko wapi Sara?"

245 Naye . . . akasema, "Yuko hemani nyuma Yako." Akasema, "Nitakurudia kulingana na wakati wa uhai." Naye Sara akacheka moyoni mwake, ndipo yule Malaika-Mjumbe ambaye Ibrahimu alisema alikuwa Mungu, akasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema . . . "

246 Hebu niwape neema kidogo hapa ndugu. Dakika hiyo, Mungu angemwua Sara kwa kutomwamini Malaika huyo, hakumwua. Mwangalieni Malaika huyo, akishuka na kumwambia mke wa Lutu asiangalie nyuma. Mnaona kilichompata, kwa kutokuamini kwake? Mnaona? Lakini hangeweza kumchukua Sara, kwa sababu alikuwa sehemu ya Ibrahimu. Na siku hizi, kutokuamini kwa Kanisa halisi la kweli, lina kutokuamini, bali Yeye hawezi kuligusa, tuko ndani ya Yesu. Mnaona? Huwezi kulichukua Kanisa bila kumdhuru Kristo; hangeweza kumchukua Sara bila kumdhuru Ibrahimu, kwa hiyo neema ilifunika jambo hilo.

Sara akaogopa, akakana; Yeye akasema, "Ulicheka."

Sasa, Yesu alisema, "Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

247 Je, uliwahi kuona kwamba *Ibrahimu* linamaanisha "baba wa mataifa"? H-a-m, katika historia yote ya ulimwengu, hatujapata kuwa na mtu huko nje Babeli, kama tujuavyo sisi, akileta ujumbe kama, akiwa na jina lile lile, tulilo nalo leo, G-r-a-h-a-m, kwa kanisa la kimadhehebu. Sasa, Kanisa lililochaguliwa, natumaini ninyi si vipofu. Sasa, angalieni, mnaona, sawasawa kabisa na Nuru ya jioni, kila kitu kikiwa mahali pake.

248 Sasa, ni nini Mungu alikuwa . . . Sasa, ni wangapi hapa ndani wanaoamini ya kwamba Ibrahimu alikuwa sahihi aliposema yule Mtu aliyesimama pale akila ndama, akinywa maziwa, akila ugali wa mahindi, na kunywa maziwa mbele ya Ibrahimu, kwamba Huyo alikuwa Mungu? Mnaamini hilo? Ibrahimu alimwita Mungu, Elohimu. Vema. Sasa, Yeye alikuwa akisema nini? Mungu, kabla ya kuja kwa Mwana wa Adamu atajidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu, kama alivyofanya wakati huo, na kufanya jambo lile lile. Kama hiyo ni kweli, acha Mungu anene.

249 Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba . . . Huenda nisiwe hapa tena, ni juu Yako, tunakaribia mwisho, Bwana. Lakini acha ijulikane ya kwamba mimi si wa bandia, nami nimesimama hapa nikisema ukweli wa Injili. Na kama Wewe utafanya mara nyingine tena, Bwana, damu yao na iwe juu . . . si juu yangu.

Tujalie, Bwana. Ujumbe Wako umetoka, na ijulikane ya kwamba Wewe ndiwe Mungu, nami ni mtumishi Wako.

250 Je, kuna wagonjwa wangapi humu jengoni? Simjui mtu hapa. Nitaangalia kwanza nione sasa kama nina hakika. Sioni mtu mmoja ambaye ninamjua kibinafsi. Sasa, kule nyuma kabisa kuna Fred Sothmann. Najua kuna baadhi ya watu ninaowajua, lakini sijui Fred yuko wapi, nilimsikia akisema, "Amina," muda mfupi uliopita, lakini hata sijui yuko wapi. Yuko huko nyuma mahali fulani, niliisikia huko nyuma. Uko wapi, Fred? Naam, huko nyuma kabisa. Ni wangapi *hapa* ndani mahali fulani mtainua mikono yenu kwamba siwajui? Hebu tuone. Hatufahamiani kabisa, inua mkono wako. Vema, hiyo hapo.

251 Nitatumainia neema ya Kristo. Nitaugeuza mgongo wangu, kuifanya tu Biblia . . . si kuwa mcheshi, bali kumtumikia Mungu. Nataka baadhi yenu mzungumze na Yeye na kugusa vazi Lake.

252 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Ni sawa, mnaona.) Sasa, watasogeza marimba hapa, kwa muda mfupi tu. Watakuwa na, mstari wa maombi. Lakini kwanza, nataka . . . ninachojaribu kupata, ni kumwacha Roho wa Mungu . . . Nitawaombea na kuwawekea mikono, nami ninataka muone ya kwamba upako wa Kristo haushindwi.

253 Ndipo, maskini mwanamke Mkatoliki, kule chini Santa Maria, naamini ndivyo ilivyokuwa, hivi majuzi alipitia hapa. Naye akapitia hapa, alipofika mstarini, akaja, akasema, alikuwa Mhispania, alizungumza kigeni, akasema, "Ninajua kwamba hungeweza kufanya hivyo, na ninajua kwamba si wewe, ni Mungu. Niwekee mikono, nitakuwa mzima." Akaupokea papo hapo, papo hapo ulikwisha, mnaona, imani, kuamini.

254 Sasa, mtu fulani aamini. Kuwa na imani. Ikiwa Yeye atafanya hivyo, hivi ninyi . . . itawafanya kuamini? Je, mtaamini? Ninangojea tu kuona kile Yeye asemacho, mimi—mimi ni mwanadamu.

255 Mnaiona hiyo Nuru? Maskini msichana anayeketi papa *hapa*, hatufahamiani, lakini Mungu anakujua. Una matatizo, ulikuwa na nimonia au kitu fulani kwanza, ilikuacha huku, umevurugika kabisa. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Ikiwa hatufahamiani, punga mkono wako namna *hiyo*, hatufahamiani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Hilo lingekusaidia? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Binti Graham. Ikiwa hiyo ni kweli, punga mkono wako. Wewe mwamini tu Mungu.

Uwe na kicho. Usiwe na shaka, amini.

256 Moja kwa moja nyuma *kule* kwenye kusanyiko, kule nyuma kwenye kile kibanda kidogo kule nyuma, mnaona ile Nuru inayoning'inia pale? Ni mwanamume, mwanamke, mwanamume, wote wawili; wanaomba. Ni jambo baya jinsi gani! Ni roho mweusi, kifafa. Bw. Higgins, amini kwa moyo

wako wote, na kitu hicho kitakuacha; Bibi Higgins, mwekee mikono, amini kwa moyo wako wote. Mungu, namkemea huyo ibilisi. Mwachilie katika Jina la Yesu Kristo!

257 Je, mnaamini, Bibi Higgins na Bw. Higgins, kwamba amewaacha? Inua mkono wako kama unaamini. Mungu awabariki. Hatufahamiani, kama hiyo ni kweli, punga mkono wako tena.

Sasa, aminini. Waligusa nini? Aminini, msitie shaka.

258 Mama *huko* nyuma mwenye ugonjwa wa kike, akiomba Mungu amponye, amini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya ugonjwa huo wa kike. Binti Stanley, hutoki hapa, unatoka Idaho. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ikiwa hatufahamiani, punga mkono wako. Ikiwa hiyo—ikiwa hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako, punga mkono wako tena. Nenda zako nyumbani, uwe mzima, Yesu Kristo anakuponya.

Mnaamini?

259 Papa *hapa*, mwanamke, mwenye fadhaa, matatizo, akimwombea mume wake pia, ana ugonjwa wa macho yake. Hiyo ni kweli. Bwana Griggs na Bibi Griggs, unaamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu atakuponya? Vema, amini. Je, mimi ni mgeni kwako? Punga mkono wako. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki, nenda ukapokee uponyaji wako.

260 Vipi kuhusu huko juu kwenye roshani? Mnafikiri mko mbali sana? Kamwe msiwazie hilo. Nawapa changamoto mwamini.

Kuna mtu anayeugua yabisi kavu. Bw. Peters, amini kwa moyo wako wote. Simama kwa miguu yako, Yesu Kristo anakuponya.

Amini! Unaamini? Sasa, jaribu kuficha kitu. Ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

261 Loo, Yeye yuko hapa! Yeye ni Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho. Yeye ndiye Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, Nyota Ing'aayo ya Asubuhi. Yeye ndiye wa Kwanza, wa Mwisho, Yeye aliyekuwako na aliyeko, na atakayekuja. Yeye ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, Yule aliye hai anayeishi milele; Yeye hajafa, Amefufuka tena; Kuja Kwake kumekaribia. Tubu, ili kutokuamini kwako kufutiliwe mbali, asije akakukuta umechoka.

262 Ee Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, uturehemu! Loo, ungeweza kufanya nini zaidi, Bwana? Jalia, Bwana, ya kwamba kila mtu hapa ataipokea sasa. Na wakati Roho Wako akiwa juu yetu, Bwana, jalia Roho Wako Mtakatifu aje sasa na kufanya kazi inayopaswa kufanywa. Ninaomba katika Jina la Yesu.

263 Kabla sijadhoofika sasa. . . Ninamwona akifanya jambo lingine pale *pale*. Kabla sijafika mbali sana, ninataka tu wale walio na kadi za maombi wasimame kwenye safu hii. Nasi

tutashuka moja kwa moja, au mnataka . . . ? Kote hapa? Vema. Wasemaje? Sehemu hii tu pamoja na kadi yako ya maombi, jitokeze. Sasa, nitaninii . . . Upande huu . . . Na kisha, acha mtu mwingine aite sehemu hiyo nyingine, ghorofani, na kwenye safu. Hebu . . . Je, ni wangapi walio kwenye kibanda hicho humo ndani? Sitaki kuendelea kuzungumza, sitaki, nataka Hii, ikae juu yangu, ili kwamba ninapowawekea mikono mtakuwa mkio- . . . mtaponywa.

264 Nitawauliza ndugu zangu, ili kusanyiko lione ya kwamba si mimi peke yangu, ndugu zangu wana haki. Njoni hapa, ndugu, njoni hapa, simameni hapa chini pamoja nami, ninyi wahudumu wote. Yeyote wa ndugu zangu huko nje, ndugu zangu wahudumu, njoni hapa kwa muda kidogo, ndugu zangu wahudumu, njoni hapa, ninawatakeni ninyi, wahudumu mnaoamini kwa moyo wenu wote.

265 Ikiwa kusanyiko hili halitakuwa na shaka, mtaona moja ya mambo makubwa sana yakitokea mtakayowahi kuona katika maisha yenu. Hiyo ni kweli. Njoni moja kwa moja huku juu. Chukueni mistari yenu, upande mmoja, mwingine. Hebu—hebu wahudumu hawa wapite wanapopitia kwenye mistari hii hapa. Hebu wahudumu waje hapa kwanza na wasimame kwenye mistari miwili moja kwa moja upande huu, wahudumu. Hilo ni sawa. Hilo ni zuri.

266 Kadi za maombi katika sehemu hii, njoni hapa na kusimama sasa. Kadi za maombi kule kwenye kibanda kile, njoni huku na msimame. Na mara tu mstari huo ukishuka, acha upande huu uje, na ule, kisha acha roshani ishuke baada yake. Na sasa, kila mtu sasa, wakati wao . . . katika nafasi yao na mahali, hebu . . . Halafu basi, ikiwa tuna wakati uliosalia, waliobaki wanakuja.

267 Sasa, tunataka kumwombea kila mtu, lakini sikilizeni, haitafaa hata chembe moja, unapita tu, unatembea, isipokuwa unaamini ya kwamba Mungu yuko hapa jukwaani na huu ndio utaratibu. Yule mwanamke alisema alimwona Bwana wetu Yesu, naye akasema alijua kwamba kama angegusa vazi Lake . . . Sasa, unaweza kumgusa. Hiyo ni kweli. Aliona alichokuwa akifanya.

268 Sasa, hawa hapa wahudumu wamesimama, watu wa Mungu waliotiwa mafuta ambao . . . kuwawekea mikono, sawa na mimi. Basi mtakapopitia hapa, basi tutaomba na kuwawekea mikono, na ikiwa unaamini, ondoka kwenye jukwaa hili, tupa fimbo zako, magongo, chochote kibaya, na uende zako ukiamini. Kamwe usiiachilie tena. Dumu nayo, haidhuru itachukua muda gani, dumu nayo kwa vyovyote vile.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapoomba.

269 Baba yetu wa Mbinguni, tutaombeana, tukiungama makosa yetu sisi kwa sisi. Mungu, jalia kila mwanamume na mwanamke aliye hapa sasa wasamehewe dhambi zao, kwa sababu mikono ya Injili itawekwa juu ya wagonjwa na wanaoteseka.

270 Mungu, kama walifanya dhambi yoyote ambayo ingewafanya wazuiliwe, ninaomba, Mungu, ya kwamba uwasamehe dhambi yao. Nasi tunajua kuna dhambi moja tu ya asili, nayo ni kutokuamini, "Asiyeamini amekwisha hukumiwa." Nasi tunajua kwamba kutokuamini ndiyo dhambi pekee iliyopo.

271 Wanaume wanaofanya uzinzi, na wanawake, na kadhalika, wanafanya hivyo kwa sababu wao si waaminio, kama wangekuwa waaminio, wasingefanya hivyo, wangekuwa wanakuamini Wewe, na kuwa na Uzima wa Milele. Ulisema, "Yeye aniaminiye Mimi, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hilo ni Neno Lako, Bwana, kwa hiyo ni kati ya kuamini na kutokuamini.

272 Mungu, jalia kila mtu anayepita hapa aweke kando kila kutokuamini. Nao watakapopitia hapa, jalia waje kana kwamba walipitia chini ya msalaba wa Kalvari wenyewe, huku Damu ikiwatiririkia. Jalia Uwepo wa thamani wa Roho Mtakatifu, ambaye ni mkuu kuliko Sulemani, usimame hapa leo katika nguvu za kufufuka kwake Kristo na kuthibitisha kila ugonjwa unaopitia hapa. Tujalie, Bwana. Na jalia wao, kila mmoja, aponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo.

273 Kila kichwa kibaki kimeinamishwa, kila jicho liendelee kufungwa, kila mtu akimwombea mwenzake. Mara tu mstari huu unapoisha, tutaitisha mstari mwingine. Vipi kama huyu angekuwa baba au mama yako hapa mstarini? Ni wa mtu fulani. Vipi kama ilikuwa ni mkeo, mumeo, mtoto wako? Ungetaka mtu aombe. Sasa, "Watendee wengine kama unavyotaka wengine wakutendee." Amina.

274 Je, utakuwa kwenye mstari wa maombi? Amini, ibilisi huyo ataondoka, Bi Pringly, na atakuondokea. Huyo ni wewe, na kifafa ndicho ulichokuwa nacho. Amini tu. Niliona kivuli hicho cheusi kikiinuka kutoka kwako na kuondoka, naomba kisirudi tena. Aliupata hata kabla hajafika kwenye mstari wa maombi. Huyo hapo. Huyo ni wewe, hilo ndilo jina lako, hiyo ndiyo shida, umekuwa nayo kwa muda mrefu. Amini tu sasa, natumaini hautarudi tena, kwako.

275 Nena kuhusu neema! Ee Mungu! Ange—angewezaje mtu yeyote kushuku? Usiwe na shaka tena, tafadhali usiwe na shaka. Sahau tu sehemu ya mwanadamu, unaona, sahau watu hawa, wao ni watumishi wa Kristo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

276 Sasa, kila mtu aombe, na hebu kiongozi wa wimbo aongoze wimbo, *Amini Tu*, kama wakipenda. Na ndugu, ninawatakeni mjongee hapa, na kila mmoja, anayepitia hapa, weka mkono wako wa huduma juu ya mtu huyo anayepitia hapa, na uombe kwa moyo wako wote sasa. Kumbuka, vipi kama huyu angekuwa

mke wako, binti zenu, mama zenu, watoto wenu? Ni wa mtu fulani, mwajua. Na hebu tuwe tu na upako, tuondolee mbali kutokuamini kwote, na kila kitu, na kusema tu, "Mungu, watakuwa wazima, hivyo tu. Watakuwa. Watakuwa wazima."

Na ninyi nyote huko nje mtakuwa mkiomba, semeni, "Amina."

277 Sasa, Mungu, ni juu Yako kufanya jambo hilo, Baba, tutakuamini, katika Jina la Yesu. Amina.

Tu . . .

. . . katika Jina la Yesu Kristo . . . Ingia moja kwa moja ndani . . .

Hao ndio aina wanaoupata. Hiyo ndiyo njia ya kuupata. [Mstari wa maombi unaendelea—Mh.]

62-0715 Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Wote Yupo Hapa
Open Bible Standard Church
Spokane, Washington Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org